Vita za kiroho

Kutembea katika Mamlaka ambayo Kristo amepatiana kwa waamini Kama washirika wa mwili wake

Ufahamu wa ngazi tatu za vita za kiroho:
Ngazi ya kibinafsi
Ngazi ya kanisa la pale pale
Ngazi ya kimataifa

Paul Galligan

Yaliyomo

	Ukurasa
Utangulizi	**3**
Ngazi tatu za vita	
Sura ya kwanza – Ngazi ya kwanza ya vita za kiroho	**6**
Ngazi ya kibinafsi – Waamini	
Ngazi ya kibinafsi – Vijana, wahuduma katika mazoezi	
Ngazi ya kibinafsi – Kumfunga mtu mwenye nguvu	
Hatua katika kutoa pepo	
Eneo la mamlaka	
Vita za kibinafsi – Kuteka nyara kila wazo	
Kuzusha kila ubishi	
Kutawala mawazo yetu	
Sura ya pili – Ngazi ya pili ya vita za Kiroho	**15**
Asili ya kweli ya kanisa	
Vita dhidi ya mamlaka na nguvu	
Waefeso kwa kifupi	
Kuna kumenyana	
Kuyatazama mavazi ya vita	
Wajibu mwafaka wa mtume	
Sura yatatu – Kukamilisha Vyote Katika Vyote [*ikiwa ni pamoja na viambatisho viwili*]	**22**
Suru ya nne – Ngazi ya tatu ya vita za kiroho	**28**
Kukabilia na nguvu na mamlaka	
Ulimwengu wa nguvu za giza za shetani	
Kikundi cha kimitume	
Silaha tatu maalum – Ufu 12:11	
Kwa damu ya mwana kondoo	
Kwa neno la ushuhuda wao	
Kwa kutopenda nafsi zao hata kifo	
Fundisho maalumu	
Tamati	
Sura tano – Kutembea Katika Ushindi	**38**
Sura sita – Shuhuda za vita katika Ngazi tatu.	**41**
Ujuzi wa Ngazi ya kwanza – Kutoa pepo	
Ujuzi wa ngazi ya pili – Kushinda nguvu katita ulimwengu wa rohoni	
Ujuzi wa ngazi ya tatu – Kukabiliana na nguvu za ulimwengu wote.	

Utangulizi

VITA VYA KIROHO

Kutembea katika mamlaka ambayo kristo amepatiana

Yesu aliwapatia wanafunzi wake mamlaka

Wakati Bwana wetu Yesu aliwatuma mitume aliwapa mamlaka ya ***"kupoza wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo"*** **Mt 10:8.** Hii ilikuwa nikatika mazingila ya kuwaambia ***"kuhubiri, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia"*** **aya 7.** Yesu, katika kuja hapa ulimwenguni, alidhihirisha ufalme wa mbinguni [unaoitwa ufalme wa Mungu katika injiri ya **Luka** na penginepo katika agaano jipya] na huduma yake iliambatana na kuyatoa mapepo. Mfano wa kipekee ni katika ukombozi wa pepo kule Gadaria. (**Luka 8:26-39)** Huyu mtu baada ya kuwekwa huru na kutumwa na Yesu, ***"Akaenenda zake, akihubiri yalivyo mambo yaliyotendwa na Yesu"*** **aya 39**

Mamlaka ya Yesu juu ya shetani

Tunajua kwamba Yesu alipingwa na shetani katika mwanzo wa huduma yake mpaka mwisho. Mara tu alipo jazwa na Roho Mtakatifu katika ubatizo wake, "***Akaongozwa na Roho mda wa siku arubaini nyikani, akajaribiwa na ibilisi Luka 2:1-2.*** Yesu alimshinda shetani mara tatu na "***Basi alipomaliza kila jaribu, ibilisi akamwacha akaenda zake kwa mda" aya 13.*** Yesu alipofikisha mwisho wa huduma yake, alisema "***Mimi sitasema nanyi maneno mengi tena; kwa maana yuaja mkuu wa ulimwengu huu, wala hana kitu kwangu"*** **Yohana 14:30.** Paulo anakielekeza kifo cha Yesu kwa ***"Wenye kutawala dunia hii"*** **1 Kor 2:8.** Hata kama Yesu ***"alitolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa na kwa kujua kwake tangu zamani… mkamwua"*** **Mdo 2:23.** Ilikuwa ni kufufuka kutoka kwa wafu kulikotangaza ushindi wake kamili juu ya ibilisi.

Katika huduma yake Yesu alikabili wa na mapepo na kutambuliwa nao, lakini Yesu alitumia mamlaka yote juu ya mapepo na nilazima yangemtii. Tukitazama tena katika kisa cha mapepo cha gadarini, Yesu alivuka bahari kuja katika mji wa Gadarini, **"*Ikashuka tufani juu ya ziwa, chombo kikaanza kujaa maji wakawa katika hatari"*** **Lk 8:23.** Yesu "***Akaukemea upepo wa msukosuko wa maji, vikakoma kukawa shwari"*** **ya 24.** Nidhahili kuwa nguvu za mapepo kule mji Gedarini zilijua ya kuwa Yesu anakuja na zikajaribu kumuangamiza alipokuwa akivuka bahari. Nia ya Yesu ilikuwa ipi- alikuwa amelala!

Kuna mambo mengi ya ndani katika hadithi hii yanayotufunulia mamlaka kamili aliyo nayo Yesu, Mwana wa Mungu aliyo nayokatika upeo zote za mapepo na amepatiana mamlaka hayo kanisani.

Katika fundisho hili ninakusudia kuonyesha vita na shetani katika ngazi tatu. Kuna ngazi tatu wazi za vita za kiroho zilizo funuliwa kwetu katika maandiko na katika miaka Bwana Mungu amenipa ujuzi katika kila ngazi kama vile nimeendelea kukua katika huduma.

Ngazi tatu za vita za kiroho

Hizi ngazi tatu ni:

- Ngazi ya kibinafsi,
- Mwili wa waumini chini ya uongozi wa wazee wa mji au eneo,
- Kanisa la Kimatafa au ulimwengu wote chini ya uongozi wa mitume na manabii.

Hata hivyo haya maeneo ya upinzani wa kiroho kwa waamini/ kanisa, zinashikana. **Shetani hapuuzi kikamilifu mashambulizi yake kwa watu binafsi, kanisa la pale pale na huduma za kimataifa za kiutume.**

Ni jambo la muhimu kwetu kutambua pahali petu katika mwili wa Kristo na kujua msimamo wetu ndani ya kristo.

- Kama mwaamini binafsi,
- Kama mshiriki wa ushirika wa kanisa
- Kama sehemu ya ***"jengo lote limeungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana"*** **Waefeso 2:21.**

Maandiko yasema "***Kwa kusudi hili mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za ibilisi"*** **1 Yohana 3:8.** Tunapokuja kulijua neno la Mungu kwa kufunzwa vyema katika neno [**Yesu ameamuru katika Mathayo 28:19-20]** tunatambua kuwa tunaweza kutembea katika ushindi na uhuru katika Kristo katika kila ngazi.

KRISTO AMEZIVUA MAMLAKA YOTE NA NGUVU

Nia muhimu sana kuwa na ufahamu wa "***Kristo ndani yetu"*** Maandiko yanasema yakuwa Kristo, aliye ndani yetu, ***"akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo"*** **Wakolosai 2:15**. Maelezo haya yana nguvu sana na wazi! Kulingana na mandiko, mamlaka na nguvu zimevuliwa kupitia Kifo cha Yesu juu ya msalaba na kufufuka kwake siku ya tatu.

Neno hili mkogo pengine inaonyesha ushindi wa Warumi wakiambatana kote Rumi kwa Jemedari aliyeshinda au liwali mwenyewe baada ya kampeini ya ushindi wa wanajeshi kutoka mkoa wa bali. Jemedali aliyeshinda na jeshi lake waliambatana kote mitaani na mateka walielekezwa wakiwa wamefungwa na wakiwa uchi. Raiya wa kirumi wamewachapa na viboko na kuwarushia vitu, Mkogo kama huo unatupa ufahamu juu ya ushindi kamili wa Yesu juu ya mamlaka na nguvu za giza.

Kristo ameketi juu sana

Paulo anatuombea tujue ***"ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo"*** **Efe 1:19.** Hii ni "***Kwa kadiri ya utedaji wa nguvu za uweza wake; alioutenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wakiume katika ulimwengu waroho.*** **Aya 20.** Kristo ameinuliwa na kuketishwa katika enzi. Yeye ni Masihi, aliyepakwa na hatima yake kuwa mwana aketiye katika enzi ya Daudi milele.

Ameketishwa ***"juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na ushultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni huu tu, bali katika uliwengu ujao pia"*** **aya 21.** Huu ni uhakika wa kuwa kanisa imeng'ang'ana katika kufahamu na kuelewa. Kumekuwa na kutoelewa juu ya via za kiroho katika ulimwengu wa rohoni na wengi wamefundisha juu ya njia ya

kushambulia nguvu na mamlaka na kanisa, wakitafsiri isivyo faa kung'ang'ana alikozungumzia mtume Paulo katika **Efe 6:12.** Maandiko haijatuelekeza kwenda tukitafuta kupigana na nguvu na mamlaka na wale wanafanya hivyo wataugua kama wana wa Skewa walivyo ugua katika **Mdo 19** kwa kuwa hawakuelewa mamlaka yao ndani ya Kristo.

Kanisa limeketishwa pamoja na Kristo

Kristo amepatianwa kanisani kama ***"kichwa cha yote"*** Mungu ***"akavitia vitu vyote chini ya miguu yake"*** **Efe 1:22.** Kristo ameinuliwa **juu zaidi;** Ameketishwa na kanisa ***"ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote"*** **aya 23** Hebu ukweli wa neno hili uwe hakika kwetu.

Katika **Wakolosai 3:1-3** Paulo anatupatia funguo za kutambua sehemu yetu katika Kristo, "***Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yafuateni yaliyo juu, Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu.yafikirini yaliyo juu, sio yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo"*** Kanisa ni mwili wa Kristo na kanisa ***"Alitufufua pamoja naye na kutuketisha katika ulimwengu waroho, katika Kristo Yesu"*** **Efe 2:6.**

Kama kristo ameketi juu zaidi na kanisa ni mwili wake na limeketishwa naye kwa hivyo sehemu yetu ni ipi juu ya nguvu na mamlaka? Jawabu ya haya inapatikana katika maandiko. Sehemu yetu katika Kristo ni kama ilivyoandikwa na tunapoweka mawazo yetu juu ya mambo hayo, maisha yetu yatafichwa katika Kristo.

FUNGUO ZA USHINDI NI KUJUA YA KUWA TUMEKETISHWA NA KRISTO KATIKA ULIMWENGU WA ROHONI, JUU ZAIDI YA MAMLAKA YOTE NA NGUVU

Sura Ya Kwanza

NGAZI YA KWANZA YA VITA ZA KIROHO

NGAZI YA KIBINAFSI – WAAMINI

Huu ni upeo ambao amepewa kila mwamini na Yesu Krtisto katika **Mariko 16:17 "*Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo".*** Kama muamini akisumbuliwa na pepo au ashambuliwe, mwaamini ana mamlaka ya kukataana na pepo hiyo na kuiamuru kuondoka.

Kama kuna pepo inakaa ndani ya mtu basi mwaamini ana mamlaka kutoka kwa Yesu kuiamuru kutoka katika Jina la Yesu.

Kutoa pepo sio rahisi vile kila mara au vyepesi lakini hakuna shaka kwamba Yesu amepatiana mamlaka kwa kila mwamini. Fahamu ya kuwa mamlaka yanapeanwa kwetu kikamilifu tunapo vikwa na Roho Mtakatifu.

Wakati Yesu alikuwa akiwafunza wanafunzi aliwapa mamlaka dhidi ya adui (**Luka 10:17-20),** Lakini wanafunzi walipojazwa na nguvu siku ya pentekote **(Mdo 1:8, 2:4),** kisha mamlaka ya Masihi ikawa ndani yao.

Mamlaka katika jina la Yesu.

Kuna mamlaka katika Jina la Yesu ya kuyatoa mapepo.

Ushuhuda: Wakati nilipokua nikimwendea Yesu kabla ya kuzaliwa mara ya pili, nilikuwa nikisoma injiri na rafiki akanijia aliyekuwa ameteswa sana. Akakaa kwa nyumba yetu na baada ya siku chache ikaelewa katika nyumba yetu kuna pepo kwa ajili yake. Nilielewa nilitakikana kumfukuza atoke kwa nyumba yetu, katika kuyatenda hayo, ikanijia nimtafute rafiki yangu alinena neno la Bwana na alipofanya hivyo, yule pepo aliondoka mara moja. Nilijua kwa kuwa amani iliturudia na tukarudi kwa nyumba na rafiki yangu hakugandamizwa tena. Hata kama mtu haja okoka, Roho wa Mungu aliniongoza, kwa maana nilikuwa nikilisoma neno, kumwona rafiki yangu akiwa amesetwa huru katika jina la Yesu. Mda mfupi baada ya tukio hilo niliokoka na tangia wakati huo nimeshuhudia mapepo wakitoka kwa jina la YESU.

KUTII NDIO UFUNGUO WA USHINDI

Mungu anatuhakikishia kwa neno lake yakuwa tuna ushindi juu ya shetani, lakini ushindi huo unakuja kwa mtu:

- Ambaye anamtii Mungu na
- Ambaye amejitisha vyema kwa mwili wa Kristo

"Basi mtiini Mungu, mpingeni shetani naye atawakimbia" **Yakobo 4:7.** Muamini hataweza kumpinga shetani asipokuwa tu amejitiisha kwa Mungu. Wengi wamefanya makosa ya kujaribu kumtoa pepo kabla ya maisha yao hayajatiishwa kwa Mungu. **Kumtii Mungu inamaanisa kutembea katika utiifu kupitia imani katika neno.** Petro pia anatuambia tutii ili tuweze kupokea neema kutoka kwa Mungu, Kujinyenyekesha ***"Chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake"*** **1Petro 5:6**.

Tunapo kua ndani ya Bwana, **utiifu unakuwa ni sehemu ya muhimu sana katika maisha yetu.** Utiifu kwanza ni kwa Mungu na tunafika katika utiifu kwake kupitia imani katika

neno lake. Hata hivyo mamlaka yetu inakua tunapokua katika utiifu, na utiifu kwa Mungu ni katika mazingira ya kuwa washiriki wa mwili.

***"Vivyo hivyo ninyi vijana, watiini wazee, Naam, ninyi nyote jifungeni unyenyekevu"* 1 Petro 5:5a**. Utiifu katika mwili kwanza ni kwa wazee, walio wazee kwetu katika asili na wale wazee katika Bwana.

Pili kila mmoja wetu, Kama tu wazee au vijana wakristo, ni lazima tuyenyekeane mmoja na mwingine. Paulo anadhibitisha hili katika **Efe 5:21** ambapo anazungumza juu ya maisha yaliyo jaa Roho, ***"Nyenyekeaneni katika kicho cha Bwana."***

Niyakupendeza kujua kuwa ni katika mazingira ya unyenyekevu yakuwa wake wanaambiwa yakwamba ***"watiini waume zenu kama kumtii Bwana"* aya 22.** Shetani angepata nafasi ndogo ya kuingilia ndoa zetu ambapo mume mumejinyenyekesha ndani ya mwili wa Kristo vyema kwa maana mke angeliweza kunyenyekea kwake kama kwa Bwana na shetani atawakimbia.

Kuomba, kuthibitika katika imani

"*Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mstaki wenu ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka – zunguka, akitafuta mtu ammeze, Nanyi mpingeni huyo, mkiwa thabiti katika imani, mkijua kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani"* 1 Petro 5:8-9. Kushambuliwa kutoka kwa shetani na kujaribiwa ni jambo ambalo kila mmoja anapitia na inaleta mateso. Lakini neno la Mungu latuahidi yakuwa tukimpinga shetani, atatuondokea. Katika hali hii upizani wetu una msingi katika kiasi na kukesha na kuthibitika kwetu katika imani. Kiasi na kukesha inazungumza juu ya **maisha ya maombi** na hakika maisha ya maombi inamaanisha kurejerea maandiko kwa kuelekezwa.

Kusimama katika imani ilionyeshwa kwanza katika agano la kwanza katika siku ya pentekote ***"wakawa wakidumu katika fundisho la mitume"* (Mdo 2:42) *"Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Mungu"* Warumi 10:17.** Tusikiapo neno na kuliamini tunatiwa nguvu ya kumpinga shetani.

Kustahimili katika mateso

Petro anaendelea kutuahidi ***"Na Mungu wa neema yote, aliyewaita kuingia kwenye utukufu wake wa milele katika Kristo, mkiisha kuteswa kwa mda kidogo, yeye mwenyewe atawatengeneza, na kuwadhibitisha, na kuwatia nguvu"* 1Petro 5:10.** Kuteseka kwa sababu ya imani na kupitia majaribu ambayo yanaletwa na shetani kinyume chetu hayawezi kuepukika nani ya muhimu katika kukua kwetu katika Kristo na kuweza kufika katika utimilifu na kuhisi utukufu wa Mungu katika Kristo Yesu. Hata hivyo shetani anaweza kupingwa na lazima atuondokee. Kuteseka haswa ni kushinda ubinafsi na mwili.

Uzoefu wa Yesu

Wakati Bwana Yesu alipofika katika utimilifu wa uwana katika ubatizo wake, kupokea Roho bila kipimo, hatua ya kwanza katika huduma yake ilikuwa ni kuelekezwa na Roho katika jangwa ili akajaribiwe na shetani (**Mathayo 4:1).** Makabiliano hayo yalikuwa ni katika ngazi ya kibinafsi kwa Yesu. Yesu alipata ushindi kwa kuuchukua ***"upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu"* (Efe 6:17)** Neno la kiyunani '**rhema**' ni neno katika **aya** hii na pia neno lililotumika katika **Mathayo 4:4 *"Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo kwa kinywa cha Mungu".***

Yesu alionyesha jinsi ya kutumia upanga wa Roho kikamilifu kwa kujibu mara tatu na neno *lililotoka ndani yake,* lililo huishwa ndani yake. Shetani alikuwa akinukuru kimakosa neno lililoandikwa, lakini kwa Roho Yesu akaleta neno lililo huishwa (kutoka ndani yake), lililompa ushidi dhidi ya shetani. Alikuwa akimpinga shetani kwa kunyenyekea kwa Mungu na kwa kusimama imara katika imani. Twaweza kusema alitumia ***'ngao ya imani'*** **Efe 6:16** ***"ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya Yule mwovu***".

Yesu alipitia wakati wa mateso hata kama vile mtume Petro anatuonya kwamba wote tutapitia mateso kwa sababu ya mashambulizi ya shetani. Baada ya hayo yote **"wakaja malaika wakamtumikia" Mathayo 4:11**

NGAZI YA KIBINAFSI – VIJANA: WAHUDUMA WAKIJIFUNZA

"*Ndipo wale sabini waliporudi kwa furaha, wakisema, Bwana, hata pepo wanatutii kwa jina lako"* Luka 10:17. Hapa tunaona wanafunzi wainjilisti au mashahidi walioinuliwa na Yesu, wakitoka nje na mamlaka ya Yesu, walikuwa na mamlaka dhidi ya shetani**. Aya 19** Yesu akasema kwa hao wanafunzi ***"Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za Yule adui, wala hakuna kitu kitakacho wadhuru***," Yesu anasema na wale mashahidi sabini aliokuwa amechagua na kuwatuma nje (**aya 1),** Baada ya kuwapa mafundisho ya kimsingi na mwelekeo wazi jinsi ya kufanya huduma ambayo walikuwa wafanye **(Lu.10:2-12)**

Shetani hawezi kukudhuru

Mamlaka ambayo Yesu aliwapatia wale aliowatuma kwa huduma ilikuwa kamili ya kwamba shetani hangewaumiza katika kuwaadhibu. Wakati mwingine watu husema, 'lazima niwe ninafanya kitu chema kwa sababu shetani ananipa wakati mgumu'. Hapana, taarifa isiyo sahihi! Yesu alisema kama unatenda kitu kwa sababu yake, hivyo anakupa mamlaka dhidi ya nguvu zote za shetani na hawezi kukuumiza. Kama tunaumizwa na shetani ni kwa sababu hatujajifundisha kushinda.

Kumshinda Yule muovu.

Mamlaka nyiingine ambayo Yesu aliwapa wale sabini ambao walikuwa wahuduma katika mafundisho ilikuwa ni kushinda au kukanyaga nguvu zote za shetani. Mamlaka haya siotu ya kutoa pepo lakini ni mamlaka ya **kushinda nguvu zote za shetani**, wakati nguvu hiyo inakuja kinyume cha wanafunzi, 'vijana' wale wanaoanza kufanya kazi katika huduma. Vijana ni wale ambao wanaweza kumshinda yule muovu kwa sababu neno la Mungu linadumu ndani yao. Yohana anawaandikia vijana akisema ***"mna nguvu, na neno la Mungu linakaa ndani yenu, nanyi mmemshinda yule muovu"*** **1Yohana 2:14.**

Kwa neno la Mungu likidumu ndani yenu

Inafikia wakati ambapo mwanafunzi anaanza kuhudumu. Mwanafunzi yuko tayari kuhudumu wakati neno la Mungu linadumu ndani yake. Nguvu huja kwa kufahamu neno na hiyo nguvu inamuwezesha mwanafuzi kuanza kuhudumu kwa sababu anajua ushindi dhidi ya shetani. Funguo za kumshinda shetani nikuwa na neno la Mungu likidumu ndani yako.

Ushuhuda wa Philipo

Wakati Philipo, mwanafunzi aliyekuwa amewekwa wakfu kama shemazi (**Mdo 6)** alienda Samalia, aliweza kuhubiri ***"Habari njema za ufalme wa Mungu na jina lake Yesu Kristo"*** **Mdo 8:12.** Na akafanya kazi kwa mamlaka meingi, ***"Kwa maana pepo wachafu wakawatoka wengi waliopagawa nao wakilia kwa sauti kuu" aya 7.*** Ushuhuda wa Philipo ulikuwa yakwamba

alikuwa mtu ***"aliyeshuhudiwa kuwa mwema, mwenye kujawa na Roha na hekima"*** **Mdo 6:3.** Alikuwa amechaguliwa 'kuhudumu mezani' Lakini kwa sabadu alikuwa mwanafunzi mwenye bidii pamoja na mtume, aliweza kutoka nje kwa huduma yenye nguvu, sio tu kwa kutoa mapepo kutoka kwa watu lakini kushinda ***"Nguvu zote za adui"*** Katika mji wote wa Samaria.

NGAZI YA KIBINAFSI – KUMFUNGA MTU MWENYE NGUVU

Katika **Mathayo 12:29** Yesu anasema ***"Ama awezaje mtu kuingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuviteka vitu vyake, asipo mfunga kwanza yule mwenye nguvu".*** Inamaanisha nini kumfunga mwenye nguvu?

Mtu mwenye nguvu ni nani?

Yesu alimponya mtu aliyepagawa na pepo, kipofu na bubu **(aya 22).** Mafarisayo wakamlaumu Yesu kwa kutoa pepo kwa nguvu za beelzeburi mkuu wa pepo. Yesu akawaambia mafarisayo, nyumba yo yoyote ikifitinika juu ya nafsi yake, haitasimama (**aya 25).** Yesu anazungumzia roho ya pepo ndani ya **nyumba**. **Nyumba hii ni maisha ya mtu binafsi,** sio mamlaka katika ulimwengu wa rohoni.

Wakati mtu anapagawa na pepo, anahitaji kukombolewa kutokana na huyo pepo. Yesu alisema wazi ya kwamba twafanya haya '**kwa kumfunga mtu mwenye nguvu'** [roho chafu] kwanza na kisha kwa **makubariano na huyo mtu**, toa pepo. Mtu mwenye nguvu anayesungumziwa hapa ni pepo mwenye nguvu katika ngazi ya mwanadamu, sio katika upeo wa ulimwengu wa rohoni. Huu ni ukombozi wa mtu binafsi. Yesu alimuweka mtu huru kutoka kwa roho ya upofu na ububu. Akasema, yakwamba amemfunga mtu mwenye nguvu na akaviteka vyombo vyake na akamseta huyo mtu huru.

Kutakasa na kujaza nyumba

Katika **Mathayo 12:43-45** Yesu anasungumza habari ya pepo mchafu ambaye ametolewa kwa mtu binafsi. Pepo kama huyo huenda katika nchi kavu; sio sisi tutangaze mahali roho mchafu ataenda. 'Nyumba'ambayo huyo pepo ametoka yasungumzia habari ya mtu ambaye pepo ametolewa ndani yake.

Pepo anapotolewa ndani ya mtu, mtu huyo lazima aelekezwe kwa wokovu kamili, ikihusisha ubatizo wa maji, kulingana na muundo wa kimaandiko na kujazwa na Roho Mtakatifu, ili asiwe na nyumba tupu.

Mkristo anaweza kuwa na pepo?

Mtu aliyeokoka anaweza kuwa na pepo; wanaweza kuwa hawajageukia uovu kabisa, au kuna sehemu ya maisha yao ingali iko katika kifungo. Kwa mfano watu waliojipatiana katika tamaa ya kimapenzi ikihusisha picha za kimapenzi kabla ya wao kuokoka, wanaweza kuona kana kwamba hawawezi kushinda kwa maana pepo aliwaingia hapo awali na hajawatoka mara tu walipookoka. Huyo mtu anastahili atubu, anyenyekee mbele za Mungu, kukiri dhabi zao, na amtoe pepo ama atolewe, na ajazwe na Roho wa Kristo.

HATUA ZA KUTOA PEPO

Hatua zifuatazo zimetokana na ujuzi na zimepatianwa kama kielekezo kumsaidia mhuduma na mtu binafsi ambaye amesubuliwa na pepo kujua jinsi ya kufanyika huru au kusaindia kukomboa mtu mwingine.

Kutoa pepo ina ushindi wakati mhuduma [au mwamini] anajua mamlaka yake na msimamo wake ndani ya Kristo. Hapana haja ya kupasa sauti kwa pepo bali nena kwa mamlaka ndani ya Kristo. Nimeshawahi ongea na pepo kwa sauti ndogo mara kwa mara na wakati na wamenitii.

- **Thibitisha kuwa mtu anataka kuwa huru kutokana na pepo.** Niliulizwa kumwombea mwanamke wakati mmoja lakini sikuweza. Nikamuuliza kama anataka kuwa huru. Akanieleza hataki. Kutoku baliana kwake ndio sababu si kumkomboa [Yule mwanamke alibadirisha mawazo yake na akawekwa huru baadaye] Mtu mzima anastahili kukubali au kwa kukusudia atafute ukombozi. Kwa watoto, mzazi ama mwangalizi wanaweza kuwaleta kwa ukombozi.

- **Kataana na pepo ndani ya mtu na uongee na huyu mtu, lakini sio pepo.** Wakati mwingine huyu mtu anawezakuwa amechukuliwa kama kwa usingizi na pepo. Kufunga pepo sema, ‘pepo ninakufunga kwa njina la Yesu’. Baada ya kufunga pepo muite yule mtu kutoka kwa usingizi. Lazima uwe unaweza kuzungumza na huyu mtu. **usiingie** kwa mazungumzo na pepo.

- **Tafuta kujua jina la mtu na umuulize kama anataka kuwa huru. Kisha umuulize amkiri Yesu, jina lililo juu ya majina yote!** Mpaka hapo pepo anaweza kukataa na ajaribu kumzuia huyo mtu kuongea. Pepo anatakikana kufungwa kikamilifu na asiburudishwe. Amuru pepo kunyamaza kama Yesu alivyo fanya.

- **Elekeza mtu kwa ombi la kumuamuru kwa jina la Yesu, mkikubaliana pamoja yakwamba ni lazima pepo atoke.** Unaweza kueleza wakati pepo ameenda kwa amani inayokuja; wakati mwingine huwa ni kupumua kwa nguvu kutoka kwa mtu ama ishara nyingine, sio lazima asikike, Lakini utajua [kubabanua] yakuwa pepo ameenda. Katika hali zingine mtu atajaribu kutapika kwa nguvu kufukuza pepo.

- **Hakikisha huyu mtu ni mwaamini, yakwamba amempokea Yesu katika maisha yake. Kama sivyo, waelekeze kwa Yesu. Kisha waombee wajazwe na Roho Mtakatifu –** Nyumba ambayo imetakazwa lazima ijae Mungu. Kama sivyo yule pepo atarudi na wengine saba wabaya kumliko. Ubatizo wa maji ni wa muhimu kama huyu mtu hajabatizwa kama muamini.

Maeneo ya mamlaka

Kuna maeneo maalumu ya mamlaka ambayo kila mtu binafsi anastahili kuwa na ufahamu wake.

- Kwanza kila mtu ana **mamlaka juu ya maisha yake**. Hii inamaana kuwa mtu asikubaliane na ushambulizi wowote wa kiroho. Na nilazima tuzungumzie kila ushambulizi wa kiroho, tukijua msimamo wetu wa mamlaka ya Kristo katika ngazi ya kibinafsi ya vita.

- Pili, mtu ambaye **ni mzazi ana mamlaka juu ya jamii yake**. Kuna mpangilio wa uongozi ambao umewekwa na Mungu lakini mama na baba wana mamlaka makubwa ya kiroho ya kuwalinda watoto wao, kuwaleta katika uhuru wa Kristo.

- Tatu, mamlaka ya kibinafsi inahusisha **mamlaka juu ya fedha za mtu binafsi na za jamii, juu ya nyumba juu ya mali;** kama jamii ina biashara, mamlaka juu ya biashara kusimama na kupinga mashambulizi yoyote ya adui.

- Nne, mfano juu ya maeneo ya vita za kibinafsi imeelezwa katika mazingira ya shule: **mwalimu binafsi ana mamlaka juu ya darasa lake mwenyewe** kupinga kazi yote ya ibilisi, lakini hana mamlaka ya shule yote. **Mkurugenzi wa shule ana mamlaka yote ya shule**, lakini wakati mwingine baraza la shule ama idara ya Elimu ambayo imemchagua mkurugenzi.

- **Mwisho, Twatakiwa kusimama chini ya mamlaka yanayo stahili ili tuweze kufanyisha kazi mamlaka** katika maeneo ya majukumu yetu binafsi. Wakati kanisa linakuja katika mamlaka ya mpangilio wa kiutume, hapo kanisa la palepale litaweza kusimama kinyume cha shetani, sio tu kupiga bali kushinda, na mwamini binafsi atajua mamlaka yake na aweze kuishi na kutembea katika uhuru wa Kristo.

VITA ZA KIBINAFSI – KUTEKA NYARA KILA WAZO

Vita katika mawazo

Kuna kifungu chenye nguvu katika **2 Wakorintho 10:3-6** kuhusu vita. Kifungu hiki cha maandiko chazungumza juu ya vita za kibinafsi. Kimsingi haswa inazungumza juu ya vita katika mawazo yetu. **Maandiko haya hayazungumzii juu ya ngome za shetani katika ulimwengu wa rohoni,** ila kuna nguvu za mapepo zilizo kazini zikiwandanganya watu juu ya yale wanaamini.

Hata hivyo vita za Paulo zazungumza na kutuelekeza katika, ni katika mazingila ya upeo wa mawazo, hivyo ni, mawazo, kila kitu kilicho inuka, imani, na nia inayo kuja na imani hiyo. Imani ya watu hatimaye huwa na nguvu nyingi sana, kujionyesha kwenye nguvu kunakoelekeza katika kila tabia mbovu na shida za kibinafsi.

Kutembea katika Roho

"Maana ingawa tunaeneda katika mwili, hatufanyi vita kwa njia ya mwili" **aya 3.** Kwa asili sisi ni wana wa mwili; hiyo ndiyo, lakini mara tu tunapo kuwa wana wa Mungu waliozaliwa

mara ya pili, sasa tuna Roho wa Mungu akifanya kazi ndani yetu. Kwa hivyo hatupaswi kutawaliwa na kanuni za mwili na kanuni kama hizo hazina maana tunapo kuja katika kufanywa upya mawazo yetu.

"Tulikufa pamoja na Kristo kutoka mambo ya kimsingi ya mambo ya dunia" ambayo Paulo anasema ni "***maagizo na mafundisho ya wanadamu***" nani katika ***"ibada muliyo jitungia wenyewe"*** **(Kol 2:20-23).** Kabla ya kuokolewa tulikuwa ***"tukitumikishwa na kawaida ya kwanza za dunia"*** **Gal 4:3.** Mara tunapo okolewa tunapaswa ***"Kuishi kulingana na Roho"*** kwa "***kuyafikiri mambo ya Roho"*** **Rum 8:5**

Kufanywa upya mawazo

"*Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome"* aya 4. Roho wa Kristo hutupa silaha na huwekeza kwetu nguvu ili tuweze kushinda kanuni za mwili kikamilifu ambazo zinatawala maisha yetu kwa asili. Hutupa silaha za kiroho: Uweza wa kiroho wa kubadilishwa kupitia kufanywa upya mawazo yetu.

Kutambua ngome

Ngome ni imani iliyowekwa na muundo wa kimawazo katika maisha yetu ambayo imethibitishwa imara pengine tangia kuzaliwa, kwa mazingila na hali ya kitamaduni ambayo tumekuwa ndani yake. Twapaswa kuzusha kila ngome katika mawazo yetu na hekima na nguvu za Mungu.

Ngome hizi zaweza kuwa ni **Mambo mazito ya ndani ambayo yamewekwa ndani yetu tangu kuzaliwa,** ngome kama za rangi na weupe, weusi. Zaweza kuwa za kiutamaduni, kitaifa, kabila, dini [Katoleki walipokataana katika Ireland kasikasini], dini au imani mkusanyiko [kiislamu na kikiristo ulimwengu kote]

Watu wanachukulia ngome hizo kimzaha na hawaulizi uhakika wazo. Tumekuwa na nia hiyo na imani, watu wamefanya mambo na hata wameua, kwa sababu ya ngome hizo.

Ngome hizi ziko katika maisha ya waumini na Paulo anasema yakuwa tuna nguvu za Mungu ndani yetu ya kuvuta chini ngome kama hizo. Twapaswa kuitazama upya mioyo yetu na mafikira na kuwa watiifu kwa injiri.

Neno la Mungu – silaha yenye nguvu

Ni neno la Mungu ambalo ***"lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili"*** Na ***"lina uwezo wa kuchoma hata kugawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyo ndani yake, tena lijepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo"*** **Ebr 4:12.** Hazipo nguvu zingine amanjia yeyote hapa ulimwenguni ambayo ina nguvu za kuyafanya haya. Kwa hivyo silaha yenye nguvu sana ambayo Mungu ametupa ni neno la Mungu, Biblia, neno lililo andikwa la Mungu. Hapana jia ingine ya ziada ila mwalimu anafunza neno kwa waumini. Niya muhimu sana kwa waamini kuyajua maandiko kwa moyo, hivyo kuwa na upanga ukatao kuwili.

Nikupokea neno la Mungu katika 'roho na kweli' na kujua "***utu mpya, uliuumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli"*** **Efe 4:23-24**. Mawazo yetu yanafanywa upya kwa neno la Mungu tunapoitoa ***"mili yetu kuwa dhabihu iliyo hai"*** **(Rum 12:2)**, ***"Yafikirini yaliyo juu"*** **(Wakolosai 3:2).**

Kuangusha mawazo - 2 Kor 10:5

Mawazo yazungumzia imani yetu tunayoshikilia au maoni juu ya mambo, kwa mfano mafundisho ya mabadiliko ya mazingira au imani tofauti tofauti juu ya nyakati za mwisho kanisani. Watu wanaoamini imani mbaya wanataka kutetea kila kitu.

Haya ni mabishano katika mawazo yetu na pia Paulo anasema ni lazima tuyaangushe chini. Nguvu ni neno lililo jawa na roho, likifuatishwa na maombi ya aina yote katika Roho (**Efe6:18). "*Na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa ndani, liwezalo kuziokoa roho zenu, lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikizaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu"* Yakobo 1:22-23.** Wengine wanataka mabishano ya Biblia, na vile inavyosema, lakini ni lazima maandiko yawe hakika kwetu, neno tulipokealo ambalo linatuokoa.

Ibada ya kweli ya Mungu

***"Kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu"* 2 Kor10:5. '**Kitu kijiinuacho' chaweza kuwa ni kiburi chetu na mambo ya kiburi, maoni, nia, katika agano la kale, baada ya utawala wa mfalme Daudi, kuna kuendelea kutajwa kwa 'maeneo yaliyo inuka' wakati wafalme wa kufanya upya waliketi katika enzi waliharibu ibada ya sanamu katika maeneo yalioinuka lakini mara kwa mara ibada ya YAHWEH iliendelea katika mahali palipoinuka, ambapo neno la BWANA lilikuwa limeweka wazi yakuwa ibada ya YAHWEH ilikuwa ifanyike katika uwepo wake [Hema na Hekalu].

Watu wa Mungu wako vile vile leo ya kuwa kila kikundi, kila dhehebu, zinaabudu kwa njia zao, katika pahali pao na njia mwafaka imepeanwa sawa kwa mafundisho na tabia kuhusu kanisa la Yesu katika agano Jipya. Ni mpaka tu mafundisho ya kiutume yatakaporejeshwa na kuzingatiwa, ambapo patakuwa na kuangusha kwa maeneo yaliyoinuka na watu wa Mungu watarejerea kwa ibada ya kweli ya Baba katika Roho na kweli **(Yohana 4:23-24)**

Kutawala mawazo yetu

***"Na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo"* 2 Kor 10:5**

'Kila fikira' hivyo ni, mambo ambayo tunaweka mawazo yetu kwayo; huu ni mvutano wa kimawazo ambayo yanaweza fanya kazi kama msukumo, au kifaa cha mawazo ambacho tunafanya kazi kwa njia tofauti tofauti. Ni kitu ambacho kinasukuma mtu kufanya mambo na matokeo inamsababisha mtu yule atende kwa njia mbaya, ikielekeza kwa kung'ang'ana na kuhukumika.

Fikira sio pepo ambayo inatakikana kutolewa, andiko hili lazungumzia kufikiria kwa watu na utendaji kutokana na mawazo maovu. Paulo anasema kuwa kila mmoja wetu anauweza wa kuvizusha vitu hivi chini na kuvileta katika utiifu wa Kristo. Twapaswa kuiteka kila fikira.

Kwa njia ingine, kwa kuwa watu wa kiroho, twapaswa kuyatawala mawazo yetu, tukijifunza kujihukumu kwa mtu – waroho aliye ndani yetu. Ni lazima tufahamu kuwa fikira zetu ziko katika upeo wa nafsi zetu. Usitawaliwe na nafsi yako. **1Kor 2:10-16** Inatufunza ***"roho ya binadamu iliyo ndani yake yajua mambo ya mtu"*** Na kwakuwa tumepokea Roho wa Mungu twaweza kuyajua ***"mambo tuliyo kirimiwa na Mungu"*** Mtu wa kiroho anaweza kuyatambua yote***, "wala yeye hatambuliwi na mtu."***

Kutii ni imani katika matendo

***"Tena tukiwa tayari kupatiliza maasi yote, kutii kwenu kutakapo timia"* 2 Kor 10:6.**

Jambo ni kutii kwetu kutimilisha ndani ya Kristo na tukifika hapo katika unyenyekevu wote kwake tutawasaidia wengine watoke katika kutotii kwao. Tabia zetu na neno letu zitadhihirisha na kuonyesha utimilifu wa Kristo ndani yetu.

Utiifu unahusisha 'jinsi huwa tunasikia' Katika agano jipya inazungumzia utiifu kwa jumla kuzitii amri za Mungu, na utiifu wa Krsito,

Twapaswa kwa unyenyekevu kulipokea neno la Mungu, neno ambalo ndilo mamlaka ya mwisho nani lazima tuwe tayari kutii neno tunalo lisikia – hivyo ni imani kwa matendo. Kumbuka imani huja kwa kusikia na kusikia kwa neno la Mungu **(Warumi 10:17).**

Mungu ametupa Neno Lake na Roho wake ili kutuwezesha kuzaliwa upya "***bali sio kwa ile isiyo haribika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele"*** **(1Petro 1:23).** Neno hilo linakuwa ndani yetu likituleta katika ukomavu katika uhusiano wetu na kutembea kwetu na Mungu ndani ya Roho. Huku ndiko kutembea kwa ushindi lakini funguo zake ni **'utiifu wetu.'**

FUNGUO ZA USHINDI WETU NI KUTII KWETU

SURA YA PILI

NGAZI YA PILI YA VITA

Asili ya kweli ya kanisa

Ngazi ya pili ya vita ni vita inayokuja kinyume cha kanisa la pale pale, mwili wa waumini wa mji au jiji ukifanya kazi pamoja na wazee. Katika mazingira ya biblia kanisa linatajwa kwa **kijografia:** Mji – kanisa la Efeso, kanisa la Korintho – eneo – maakanisa ya Galatia. Kanisa la jiji ni lilikutana kwa mikutano mingi tofauti tofauti ya nyumba, mashirika. Kwa mfano katika **Warumi 16** Paulo anasalimia mashirika matano kama hayo katika kanisa la Rumi: Kanisa lililoko katika nyumba ya priska na Akila **(aya 5),** Nyumba ya Aristobulu (**aya 10)**, Nyumba ya Narkiso (**aya 11),** wandugu walio na Asinkrinto (**Aya 14)** na watakatifu wote na Filologo **(aya 15).**

Katika kuwaandikia wafilipi, Paulo anawazungumzia watakatifu, na maaskofu na mashemazi **(1:1).** Kuna mambo mawili: watakatifu na maaskofu (wasimamizi) ambao ni wazee na kuna mashirika mengi ya nyumbani. Hii ni picha ya Kanisa la agano jipya. Ina utofauti mkubwa leo kanisa likitambulishwa na madhehebu maidala na majengo ya kanisa.

Kimaandiko:

- Kila muamini ni mushirika wa mwili wa Kristo (**1Kor 12:18)** amewekwa kwa mwili na Mungu mwenyewe katika ubatizo.
- Ushirika wa kawaida wa kimaandiko uliongozwa na wazee waliokuwa wamechaguliwa na mtume **(Mdo 14:23 & Titu 1:5).**
- Kanisa la pale pale la maandiko lazungumzia mwili wa waamini katika maeneo ya geografia likiongozwa na wazee waliochaguliwa na mitume.

Kwa hivyo ngazi ya pili ya vita vya kiroho kimaandiko ni kinyume ya kanisa kama hilo. Mikusanyiko na asili ya migawanyiko ya kanisa la sasa imeondolewa katika kanisa la muundo wa maandiko na hali ya vita imefanyiwa kazi katika 'jambo lisilo la kawaida' .Katika kutafuta kuangazia hali ya asiri ya vita za kiroho na kuja kutambua mamlaka ya muamini na mamlaka ya kanisa la pale pale katika Kristo, twaweza tu kuchunguza ushuhuda wa maandiko na kujifunza kutoka hapo.

Vita dhidi ya mamlaka na nguvu

Katika **Waefeso 6:12** Paulo anatutanguliza kwa vita za kiroho za hali ya juu. ***"Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho."*** Hatuzungumzi tena juu ya mapepo ambao wanawapagawa au kuwashambulia wanadamu hapa duniani, sasa tunaongea juu ya nguvu za shetani katika ulimwengu wa rohoni. Kwa kuwa asili ya adui ni wakuu na nguvu na utawala, vita ni katika ngazi ya ushirikiano, ambao ni wa kanisa la pale pale. Kanisa la pale pale katika msingi bora wa maandiko lina mamlaka ya kiutume iliyopatianwa na Kristo kupitia mitume na wazee. Mamlaka hayo yanapatia kanisa msimamo ambao wanahitaji ili kusimama na kushinda mashambulizi ya adui

Kanisa kuwekwa mahali pake

Katika **Waefeso 1** maandiko yaonyesha yakuwa Mungu ***"Akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwegu war oho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na***

ushultani, na kila jina litajwalo…akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akmweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajiri ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote" **aya 20-23.** Maandiko yanasema Mungu, ***"alitufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, Katika Kristo Yesu"*** **Waefeso 2:6.** Tunajifunza katika maandiko haya ya kuwa kanisa limeketishwa katika Kristo Yesu katika ulimwengu wa roho juu ya mamlaka yote na nguvu. Tunapo pokea ufunuo na kujua uhakika wa mahali kanisa limewekwa, Nia yetu na kukabiliana kwetu kwa vita za kiroha katika ulimwengu wa roho zinabadirika kabisa.

Ni kanisa lililokomaa ambalo linaweza kuvaa silaha za Kiroho

Fahamu kwamba fundisho la silaha za roho na ufunuo wa ninani tunamenyana naye katika ulimwengu wa rohoni [mbingu ya pili – ambapo watawala wa kishetani wako] ni sura ya **sita ya waefeso.** Kutambua kikamilifu na kufahamu mamlaka na ulinzi na vita vya kushambulia kupitia neno na maombi, watakatifu, ikihusisha wahuduma, wanatakiwa kuelekezwa kikamilifu kwa mafunzo ya udani ya ajabu ya sura ya **kwanza hadi ya tano ya Waefeso**. Hapo pekee ndipo kanisa limewekwa ili lijidhibiti kinyume cha mashambulizi ya mamlaka na nguvu. Lakini lakushangaza wengi wamefanya makosa ya kufundisha silaha za kiroho katika shule ya jumapili ya watoto wakati watu wazima hawana ufahamu wa mafundisho ya ndani na yenye kuimarisha a **Waefeso 1-5**

TAMATI FUPI YA WAEFESO

Sura ya kwanza: Baraka za rohoni, ikihushiha ***"kuwekwa kama wana"*** Ombi la ufunuo na mwangaza, na msemo waajabu wa ambapo Kristo alipo ***"juu zaidi ya Nguvu na mamlaka"***

Sura ya pili: Kwa imani tumeketishwa na Kristo katika ulimwengu wa rohoni **(aya 6**). Sisi tu kazi ya mikono yake, (**aya 10).** Tumeletwa karibu kwa damu ya Kristo; sisi ni sehemu ya mtu mmoja mpya, myahudi na mtu wa mataifa pamoja na tunajengwa kawa nyumba ya Mungu.

Sura ya tatu: Paulo anafunua mambo ya ndani ya siri na katika **aya 10** anatangaza kuwa ni wakati kanisa litatembea katika ufahamu wa siri ambapo kutakuwa na ushindi juu ya nguvu na mamlaka. Paulo anatuombea ombi lingine lenye nguvu.

Sura ya nne: Umoja wa Bwana na mwili wake, (**aya 4-6);** Ufunuo wa huduma tano ikilileta kanisa katika ukomavu katika upendo; asiri ya mtu mpya.

Sura ya tano: Kutembea katika upendo, nuru na hekima; ufunuo wa siri ya Kristo na kanisa lake.

Sura ya sita: aya 1-9 Mpangilio mwafaka katika jamii na mahali pa kazi.

Wakati kanisa linatembea katika nuru na ufunuo na utiifu kwa neno la Mungu lililofundishwa katika **Waefeso,** basi kanisa "**litasimama"** kikamilifu kinyume cha mashambulizi yote ya yule muovu.

JINSI YA KUSIMAMA KINYUME CHA UJAJA WA SHETANI – Efe 6:10-12

"*Mzidi kuwa hodari katika uweza wa nguvu zake"* aya 10. Himizo ni tuwe na nguvu katika Bwana na nguvu za uweza wake, sio kupigana na nguvu za maroho, au kupigana na shetani, lakini ni kuwa na nguvu za Bwana na kujua nguvu za Roho zilizo ndani yetu (**Efe 3:16**). Kuna aya inajulikana sana na imenukuliwa katika mazingira ya uamsho wa Pentekote ***"Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali kwa roho yangu asema BWANA wa Majeshi"* Zakaria 4:6.** Ila na kunukulu aya hii, wengi wamefundisha na kufanya kazi njia ya vita za kiroho sana sana kwenye msingi wa bidii ya mwanadamu, na ufahamu wake.

Kwa kuvaa silaha zote za Bwana

Katika **aya 11** Paulu anatuambia ***"Vaeni silaha zote za Mungu, muwezi kuzipinga hila zote za shetani"*** Twapaswa kusimama kinyume cha shetani, tukijua ya kuwa anatutafuta kila wakati. Mazingira ya maelezo ni kwa kanisa kama mwili sio kama kikundi cha watu binafsi. Twapaswa kuvaa silaha zote za Bwana. Mashirika mengi ya pale pale ni pahari pa waamini kukutana lakini Mungu anataka watu wake wakutanike kwa mpango. Kama waamini binafsi wakikusanyika tunaweza kuwa tu kundi la mawe yaliyo hai. Ni wakati tu tunakusanyika [mawe yajengwa kuwa ukuta] ambapo mwili unaweza kufanya kazi na kutimiza yale ambayo Kristo amekusudia na kuweka wakfu. Kanisa ambalo hakika limekusanyika ni kanisa ambalo litajua kuvaa silaha zote za Mungu na kuweza kusimama kwa sababu kanisa limeletwa katika ukomavu kupitia utendaji kazi wa huduma tano za mtume, nabii, mwinjiristi, mchungaji na mwalimu (**Waefeso 4:11-14)**

Kuna kukabiliana

Kuna kukabiliana kusiko kwa kawaida, ngazi ya mapepo. Kuna vita dhidi ya nguvu za angani. Tupo hapa duniani na ni wakati nguvu zinajaribu kumenyana nasi hapa ulimwenguni tunapo jaribu kutimiza utume mkuu ambapo tunang'ang'ana. Hizi nguvu zaweza kushawishi watu binafsi, serekali na viongozi. Wakati wakristo wanaanza kuinuka na kanisa kufanyika mwili unao fanya kazi kuna kung'ang'ana na nguvu. Hii inaweza kudhihirika kupitia dini za uonga zikifanyika wanajeshi kinyume cha wakristo na injiri, kupitia serekari na mamlaka wakiidhinisha na kutangaza sheria na amri za mpinga – kristo, na kupitia roho [nguvu] za Jezebeli ambaye anashambulia kanisa kwa kuligandamiza **(Ufu 2:20-26)**

Lakini tunaweza kusimama

Hata hivyo **aya11** tumeambiwa '**tusimame**' sio tunga'ngane, tufunge au tutishe. **Aya 13** kisha inasema **"Kwa sababu hivyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkisha kuyatimiza yote, kusimama."** Twapaswa '**kusimama**' hivyo ni kusimama mahali pako kwa kuwa kitu kiko kinyume chako. Wakati mashambulizi yanakuja unaweza kusimama kiyume cha nguvu za shetani, kwa maana umejifunza kusimama, Paulo anatuhimiza tena katika **aya 14 'kusimama'**

Mafundisho haya ni ya kutuwezesha kusimama na kupinga mashambulizi yoyote ya shetani. Hii sio kuongea tena juu ya vita za kibinafsi bali ni vita za ushirika zikihusisha kanisa la kijiji au mji na wazee pamoja na waumini katika kijiji hicho. Hatujaambiwa tupigane na nguvu, bali tusimame kinyume na nguvu. Yesu alitangaza katika **Mathayo 16:18 "*Nitalijenga kanisa langu, wala milango ya kuzimu haitalishind".***

Kazi yetu ni kufanya kazi katika huduma ya kuujenga mwili wa Kristo mpaka sisi wote tufike ukomavu. Tunapofanya kazi kwa njia hii ya huduma iliyopatianwa wazi na Mungu, adui

atashambulia lakini tumeagizwa katika aya hizi na katika zingine nyingi katika mahali kwingine jinsi ya kusimama katika mashambulizi ya adui.

KUTAZAMA TENA SILAHA ZETU – Waefeso 6:14-17

Aya 14-17 inaorodhesha vifaa sita vya silaha za vita na **aya 18** yatuambia kwamba sehemu ya saba ya 'kisimama' ni katika maombi: Maombi ya watakatifu wote! Maombi yote katika Roho! Ni kazi ya pamoja na matendo: **MAOMBI**

Mshipi wa Ukweli

"*Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani"* aya 14 Ukweli ni nini? Yesu alisema "***Uwatakase na ile kweli; neno lako ndiyo kweli"* aya 17:17.** Njia ya kwanza ya kusimama ni kujifunga mshipi wa kweli wa neno. Lakini ina maana gani 'kujifunga mshipi mshipi wa kweli kiunoni? Kama neno ndilo kweli hatuwezi wazi wazi kujifunga mshipi wa kweli. Nilazima tutafakari: Neno linafanya kazi namna gani kufunga viuno vyetu, kusimama kinyume cha shetani?

Petro anasema "***Kwa hiyo vifungeni viuno vya nia zenu, na kuwa na kiasi; mkitumaini kwa utimilifu ile neema mtakayo letewa katika ufunuo wake Yesu Kristo"* 1Petro 1:13.** Twatakiwa tuwe na ukweli wa neno la Mungu katika nia zetu na mawazo. Ahadi ya agano jipya ni kuwa Mungu alisema katika **Yeremia 31:31-33 "*Nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika"*** Soma, jifunze na ufahamu neno la Mungu ili liwe kwa mawazo yako. Mawazo ni lazima yafunzwe kikamilifu katika neno la Mungu. Hii ndiyo kazi ya uwanafunzi na kimsingi ni kutimizwa kwa utume mkuu **(Mathayo 28:19-20).**

Kuna mafunzo mengi katika agano jipya kuhusu nia na mawazo. Twapaswa "***Kufanywa upwa katika nia ya mioyo yetu"* Efe 4:24;** twapaswa "***kugeuzwa kwa kufanywa upya nia zetu" Warumi 12:2,*** na twapaswa "***kuyafikiri yaliyo juu"* Wakolosai 3:2.** Neno kamili kutubu ni '*kuyageuza mawazo'*.

Kama basi mshipi wa kweli utayafunga mawazo yetu, kwa nini maandiko yanasema ni **mshipi unaozunguka kiuno**? Kwa sababu watu wa kale waliamini kuwa mawazo yalikuwa katika sehemu ya chini ya mwili. Hawakudhania kuwa mawazo yawe kwenye kichwa kama mtu wa sasa anavyo ona. Watu wakale hawakutilia mkasa kwa 'kichwa' ufahanu lakini ni kwa 'ukweli wa ndani ' Neno katika agano jipya linalo tafsiliwa 'mawazo' na wakati mwingine moyo ni 'figo'. Ndiposa Paulo anasema funga viuno kwa mshipi wa kweli.

Dirii ya haki kifuani

"*Na kuvaa dirii ya haki kifuani"* aya 14. Dirii ya haki haswa inalinda sehemu ya mwili ambapo moyo upo. Ni dirii ya haki, 'haki' ni nini? Na hua tunaivaa namna gani? Tunapatiwa haki tunapokuja katika imani ndani ya Kristo "***basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo"* (Warumi 10:17).** Dirii hulinda mioyo yetu na ni ***"kwa moyo mtu huamini hata kupata haki"*** (**Warumi 10:8-10).** Haki huja kwa kuamini neno ndani ya moyo wako.

Neno linatoka kwa mawazo mpaka kwa moyo, likileta haki. Kama tukitembea kwa haki Shetani hawezi kutushtaki kwa neno lolote.

Viatu vya injili ya amani

***"Na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa injiri ya amani"* aya 15.** Viatu zazungumzia 'mwenedo wetu'. Mara tu tukiwa na neno la kweli katika mawazo yetu na unaamini moyoni mwako, basi unaweza kutembea katika ufahamu wa neno. Kutembea huku ni katika njia ya amani, na amani inapatianwa kama tabia ya ufalme wa Mungu katika Roho Mtakatifu (**Warumi. 14:17)**

Maandiko yanena, ***"Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini"* Isaya.26:3.** Injiri inaitwa injiri ya amani ***"Ni mizuri kama nini miguu yao waihubilio injiriya mema?"* (Warumi 10:15)**

Tukishajifunga mawazo kwa ukweli na kuamini ukweli wa moyo, tunaweza kuondoka tukihubiri injili ya amani. Viatu zinatuwezesha kusimama na kudhibiti mashambulizi ya shetani, na tena ni neno! Kuhubiri neno!

Mungu anaahidi amani hii kwa wale wote ***"wanauliza" kwake kwa "maombi, dua na shukrani***" **(Wafilipi 4:6)** Amani hii basi ni mlinzi juu ya mawazo na mioyo yetu, kama ilivyokuwa, ikiweka muhuri neno ambalo mawazo na moyo zimeamini.

Ngao ya imani

"Zaidi ya yote mkitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule muovu"* aya 16.** Imani inasemekana kua ngao na imani chanzo chake ni kusikia, ***"na kusikia huja kwa neno la Kristo" Warumi 10:17. Hili ni neno lililo huishwa **(Mathayo 4:4).**

Mara tunapoanza kujifunza neno kwa mawazo yetu, kuamini neno mioyoni mwetu na tunatembea katika ukweli wa neno la Mungu, sehemu hiyo nyingine ya silaha ni kulipokea neno lililohuishwa tunapo shambuliwa au kutatizwa. Ni neno la imani linalokuja ndani ya mioyo yetu kwa ufahamu ili tuweze kulitumia neno la Mungu ili kuizima mishale ya shetani inayo kuja kinyume chetu. Mishale hii inaweza kuwa kwa njia ya shaka, mambo ya kuumiza ambayo yamenenwa kutuhusu au juu yetu na mambo kama hayo.

Kumbuka ni ***"imani yetu ambayo imeshinda ulimwengu"* 1Yohana 5:4.**

Chapeo ya wokovu

"*Tena ipokeeni chapeo ya wokovu"* aya 17. Chapeo hufunika kichwa, ambayo inawakirisha hali yetu ya kukata kauli fikira, pahali pa mamlaka.

Kutoka sehemu ya silaha iliyotangulia twaweza kusema mawazo yetu yamejazwa neno na mioyo yetu inaamini neno. Sasa tunaweza kuamua maamuzi ya kiungu, ambayo ni mafikira ya mapenzi.

Tukiwa kwa vita twatakiwa kufanya maamuzi ya kiungu, tukiwa na mawazo yetu, maenzi na hisia zote zikizamishwa katika ukweli wa neno la Mungu. Twayatafuta mapenzi ya Mungu katika kila uamuzi; tuko vitani, lakini tukiongozwa na Bwana kikamilifu, tukiyanyenyekesha mawazo yetu kwa mapenzi ya Bwana, tukiongozwa na Roho Mtakatifu.

Upanga wa Roho

"*Na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu"* aya 17. Hili ni neno lililo huishwa la Mungu; **Mathayo 4:4 na Luka 4:4** inapatiana mfano mzuri wa vita za kiroho ukitumia upanga wa Roho. Yesu alitumia 'Neno lililo huishwa' ule 'upanmga wa Roho' kumshinda shetani. Elewa majaribio ya shetani yalikuwa ni katika maneno.

Vita nyingi zinatokea katika mawazo yetu wakati maneno/mafikira na maono yako kinyume, ikitustaki, ikituhukumu na kutuvunja moyo. Ni kupokea ushindi katika mawazo katika

vita hizi tunahitaji "***Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu" (Wakolosai 3:16);*** Yakuwa twahitaji kusikia ***"lile neno la imani tulihubirilo; neno lililo karibu, katika vinywa mwetu na mioyo yetu"*** **Warumi 10:8**.

Wakati Yohana alimuona Yesu katikati ya zile taa saba /vinala "***alikuwa na upanga mkali, wenye makali kuwili, ukitoka katika kinywa chake"*** **(Ufu 1:16)** Wakati Yesu alizungumza na kanisa la Pergamo alisema "***Haya ndiyo anenayo aliye na upanga mkali, wenye makali kuwili"*** **(Ufu 2:12).** Shinda kubwa mbili katika Pergamo ilikuwa ni juu ya mafundisho. "***mafundisho ya Baalamu"*** **aya 14** na ***"mafundisho ya Wanikolai"*** **(aya 15)**. Ni neno la Mungu "***lililo na nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili"*** **(Ebr 4: 12)** ambalo linaleta mafundisho ya kweli, ukweli halisi wa neno la Mungu.

Katika **Wathesalonika 2, 'yule asi'**, ***"Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa chake, na kumwaangamiza kwa ufunuo wa kuwapo kwake"*** **(2:8).** Hata hivyo kabla ya huyo kuangamizwa wengi watakuwa wamepokea ***"guvu ya upotovu, wauamini uongo"*** (**aya 11**). Vita ni katika **neno:** Ukweli au uongo. Upanga wa roho ni neno la Mungu!

Kuwaombea watakatifu wote

Hatimaye tunaulizwa kuomba "***Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote"*** **aya 18.** Tunaamuliwa kuwa katika maombi ya kuendelea kwa watakatifu wote ili kama mwili tuweze kusimama na kumpinga shetani. Haya maombi yanaweza kuwa ya kibinafsi au ya pamoja, lakini ni lazima yaongozwe na Roho. Dua zinahusisha kujitambulisha na mahitaji ya wengine na kusongea enzi ya neema kwa niaba yao.

Maombi hayahusishwi kama sehemu ya silaha. Hata hivyo ni nambari saba na katika mazingira ya silaha hizi zingine sita, pengine ndiyo ya muhimu na inafanya kazi.

SILAHA ZA ROHO KWA KIFUPI

- **Mshipi wa ukweli –** Fikiria juu ya neno la Mungu.
- **Dirii ya haki –** Tafakari juu ya ukweli wa neno la Mungu.
- **Viatu vya injiri ya amani –** Tembea katika ukweli wa neno la Mungu.
- **Ngao ya imani –** Amini ukweli wa neno la Mungu.
- **Chepeo ya wokovu –** Kulindwa kwa ukweli wa neno la Mungu.
- **Upanga wa Roho –** Ongea ukweli wa neno la Mungu.
- **Maombi –** Omba ukweli wa neno la Mungu.

Wajibu mwafaka wa mtume

Katika **aya 19** Paulo unauliza kuombewa "***Nipewe usemi kwa kufumbua kinywa changu, ili niihubiri kwa ujasiri ile siri ya injiri"***. Ili tupate ushindi katika vita hizi tulizo ndani yake, na kusonga mbele, twahitajika kuwaombea mtume na wazee waliochaguliwa na mtume ambao wanawajibika katika kulihubiri neno.

Paulo alijua ya kuwa anapaswa kunena kwa ujasiri, ili watakatifu walipokee neno na kukua ndani ya Kristo na waweze kusimama na kupinga mashambulizi ya shetani katika siku ya ubaya.

Pasipo mafundisho ya kiutume, ***"neno kamili la Mungu***" (**Mdo 20:27),** mashirika ya pale pale hayatapata ushindi katika kujikimu mashambulizi ya shetani na kudanganyika na kupotoshwa na mbinu pasipo hata kuzijua.

Nguvu za kuhubiri injili

Katika **Mdo 8** Philipo, shemazi aliyewekwa wakfu, alienda Samaria kuihubiri injiri na palikuwa na matokeo yenye nguvu. Jiji hili kuwa chini ya mchawi ambaye alikuwa ameonyesha nguvu katika Jiji hii (**10).** Philipo alikuja peke yake, akiihubiri injiri; watu wakashuhudia miujiza, uponyaji na ukomozi **(6-7),** na wengi waliamini. Hapa tunaona **kuhubiriwa kwa injiri na ishara na maajabu zikizishinda nguvu**. Mtu mmoja mwanafunzi, aliye funzwa na kuandaliwa na kutumwa na mitume na akiweza kuhubiri na ishara na maajabu na kuadhili Jiji lote. Zilikuwako nguvu nyingi na mtu wa Mungu. Alihubiri kwa wepesi ufalme wa Mungu na hata mchawi akajinyenyekesha kwa neno lake na akabatizwa **(aya 13)**

Nilazima tujue mamlaka yetu katika Kristo

Katika **Mdo 19** tunasoma juu ya Paulo katika Efeso. Katika **aya13** watu wa kijiji walisikia kuwa Paulo alikabiliana na pepo kwa jina la Yesu na wakadhania kuwa wanaweza fanya hivyo pia. Lakini walipokabiliwa na pepo, akawauliza "***Yesu namjua na Paulo namfahamu, lakini ninyi ni nani" (aya 15).*** Walijaribu kutoa pepo kwa jina la Yesu ambaye Paulo alihubiri; hawakuwa na mamlaka yao na kwa hivyo walishambuliwa wenyewe na Pepo.

Matokeo ya haya ni kuwa Jiji lote walijawa na hofu ya Bwana na jina la Yesu Kristo likatukuzwa, na "***Hivyo ndivyo neno la Bwana lilivyozidi na kushinda kwa nguvu"*** **aya (17-20)**

Paulo alikuwa akihubiri neno, akihojiana kila siku; matokeo yalikuwa kwamba upeo wa mapepo yalishindwa. Jiji likaleta shida. Nguvu za mapepo zilipita mipaka kwa kuwashambulia baadhi ya Wayahudi waliokuwa na uwezo wa kuhamisha mapepo, Lakini jina la Yesu lilitukuzwa na watu wakatoka kwa ibada ya mapepo na wakamgeukia Mungu. Hapana udhibitisho tosha wa kukataa nguvu, ni kuhubiri na kufundisha neno la Mungu tu.

FUNGUO ZA USHINDI NI KUWA PAMOJA KATIKA USHIRIKA
CHINI YA WAZEE WALIOCHAGULIWA NA MITUME;
KISHA KANISA LA PALE PALE LINA MAMLAKA
KUSIMAMA KINYUME CHA MAMLAKA NA NGUVU.

Sura ya tatu

KUKAMILISHA VYOTE KATIKA VYOTE

"*Kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote"* Waefeso 1:19b-23.

Kanisa lawezaje kukamilisha 'vyote katika vyote' kama mwili wa Kristo na hii inahusiana kwa njia gani na maelezo ambayo Paulo anatupa, akieleza kwamba Kristo ameketi 'juu sana' kuliko nguvu na utawala wa mapepo? Ili kutusaidia kufahamu vita vya kiroho ambavyo tunakabiriana navyo, tunahitaji kufahamu kwamba kuna mbingu tatu ambazo zinatajwa katika Maandiko.

1. **Mbingu za kwanza:** jua, mwezi, na nyota zilizoumbwa na Mungu; **(Mwanzo 1:14-16),** hapa ndipo tunaishi katika himaya ya asili na hapo ndipo kanisa [watu wa Mungu] wapo katika dunia.
   - **Nuru katika mbingu ya kwanza** ni nuru ya kawaida ya jua, mwezi na nyota.

2. **Mbingu za pili:** ni ulimwengu usioonekana unaokaliwa na **"*Viti vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka"* (Wakolosai 1:16).** Hapa ndipo kushindana kunakotajwa katika **Waefeso 6:12** kunaendelea. Nguvu za mapepo zinajaribu kuharibu kanisa na kupunguza ushawishi wa injili miongoni mwa watu duniani. Ni kanisa, mwili wa Masihi, ambao unatumiwa na Mungu kujulisha hekima ya Mungu ya namna nyingi na ***"Falme na Mamlaka katika ulimwengu wa roho"* (Waefeso 3:10).** Ni katika himaya hii ya mbingu ambapo shetani anafanyia kazi, anatambulika kwetu kama ***"Mfalme wa uweza wa anga, roho Yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi"* (Waefeso 2:2).**

   Ni kutoka mbingu ya pili, himaya ya mapepo na enzi, usultani na mamlaka, ambapo ndini zote za uongo zimetanda katika dunia, zikindanganya vikundi vikubwa vya watu duniani. Ndini hizi ambazo zinz majina ambayo zinaitia zote zinafanya kazi chini ya nguvu ya mapepo na haswa kutoka kwa nabii wa uongo mwenyewe (**Ufunuo 16:13).**
   - **Nuru katika mbingu huu wa pili** inatakiwa kuwa ni kanisa likisukuma hizi nguvu za giza nyuma.

3. **Mbingu za tatu:** inazungumzia mbingu ambazo hazikuumbwa ambapo enzi ya Mungu ya milele iko. Paulo anayazungumzia haya akisema, "***Mtu huyu alinyakuliwa mpaka mbingu ya tatu…yakuwa alinyakuliwa mpaka peponi"* (2 Wakorintho 12:2 na 4*).*** Hii ni himaya ya Hekalu ambayo haikuumbwa ambayo inatajwa katika **Waebrania 9:11**, "***Lakini Kristo akiisha kuja, aliye kuhani mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyika kwa mikono, maana yake, isiyo ya ulimwengu huu"*** Muandishi anaeleza zaidi katika **Waebrania 9:24**, "***Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa***

patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu”.

Yesu ameketi katika mkono wa kuume wa enzi ya Baba kulingana na **Ufunuo 3:21**, na Yesu anawaahidi washindi: “***kuketi pamoja nao katika kiti chake cha enzi”.*** Hii ndio dhawabu ya watakaoshinda, kuketi katika enzi na Yesu; kutawala na kutamalaki na Yesu, sasa.

- **Nuru katika mbingu ya tatu** ni Bwana Mungu mwenye enzi na Mwana kondoo **(Ufunuo 21:22-23)**

[Tazama Kiambatisho namba moja]

Nafasi ya kanisa

Kanisa tunalojua liko duniani, lakini kanisa hilo hilo limeinuliwa juu na Kristo ***“Akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa rohoni katika Kristo Yesu”*** **(Waefeso 2:6).** Kristo ako wapi? Ameinuliwa na ***“akamweka mkono wake wa kuume”*** **(Waefeso 1:20*);*** amefufuliwa na kuketishwa ***“juu sana kuliko ufalme wote na nguvu…”*** **(Waefeso 1:21).** Kutoka kwa haya tunaona kwamba kanisa liko duniani na mbiguni – katika mbingu ya tatu, likiwa limeketishwa pamoja na Kristo. **Hii ndiyo nafasi ya kanisa!**

Tunapofikia kujua nafasi ya kanisa kwa uhakika, mtazamo wetu katika vita vya kiroho unabadilika kwa haraka. Sio kanisa kuondoka na kufanya vita dhidi ya nguvu za mapepo. Haya ndiyo yamekuwa mazoea ya wengine, lakini sio zoezi la Yesu na mitume katika Agano jipya. Sio jambo la ramani ya kiroho! Sio mpango wa kufanya mikutano ya maombi katika maeneo ya kimkakati. Tume ni kuhubiri Kristo na ufalme wa Mungu: Hii ndiyo njia ya vita vya kiroho! Kanisa linapofikia kutambua kwamba tumewekwa nafasi moja na Kristo ‘juu sana’ zaidi ya falme na nguvu, mtazamo wa vita unabadilika kwa ule unaotekeleza ushindi ambao tayari umepatikana.

Jina la Yesu liko juu ya yote

Kama vile Paulo anatangaza katika **Wafilipi 2**, katika kueleza siri ya utauwa [Mungu alidhihiriswa katika mwili, **1Timotheo 3:16]** Mungu ***“Alimwadhimisha mno,*** **[Yesu]** ***akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba”*** **(Wafilipi 2:5-11)**

Yesu kichwa cha kanisa yuko juu ya yote, akitawala na kutamalaki kutoka kwa enzi Yake katika mbingu ya tatu. **Wafilipi** inatufundisha ya kuwa kwa sababu ya utiifu wake wa kujitolea kwa mapenzi ya Mungu, ***“Bali akijifanya hana utukufu”*** **(Wafilipi 2:7),** Yesu ameinuliwa pahali pa juu na amepewa jina ambalo liko juu ya kila jina.

Kwa yale yalionukuliwa hapo juu, Paulo pia anazungumzia himaya tatu, lakini hahusishi mbingu ya tatu katika kauli hii. Anarejelea kwa:

- ***“Walio mbinguni”*** **–** hii inaonyesha watawala wa mapepo katika mbingu ya pili
- ***“Walio chini”*****-** Hii inaonyesha wanadamu
- ***“walio chini ya dunia”*** **–** hii inaonyesha mapepo wa kuzimu

Yesu ana mamlaka yote katika kila himaya, na amekabidhi mamlaka hayo kwa kanisa lake kwa Jina Lake.

Kanisa katika ukomavu

Ni wakati kanisa linakua katika ukomavu kulingana na muundo wa maandiko ambapo kanisa litaweza kudhihirisha na kujulisha ***“Hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi…kwa falme na***

mamlaka katika ulimwengu wa roho" **(Waefeso 3:10).** Hivi ndivyo kanisa ***"litakamilika kwa vyote katika vyoye"*** **(Waefeso1:23).** Hivi ndivyo nguvu za mapepo katika maeneo ya mbinguni yatashindwa na kuletwa katika utiifu kwa kusudi la Mungu la milele. Ni kwa kuhubiri na kufundisha Yesu aliye Masihi! **(Mdo 5:42).** Ni kwa kupitia kuhubiri Kristo! (**Mdo 8:5**). Ni kupitia ***"upuzi wa lile neno lililohubiriwa"*** **(1Wakorintho 1:21)** kwamba kusudi la Mungu katika kuleta wokovu kwa mwanadamu inafunuliwa.

KANISA HILI LINA SURA GANI?

Msingi wa pekee ni Yesu Kristo

Limejengwa kwa msingi wa pekee, Yesu Kristo. ***"Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo"*** **1Wakorintho 3:11.** Ufunuo wa Yesu Masihi, Mwana wa Mungu ndiye msingi wa kanisa **(Mathayo 16:18).** Huu ndio **"Mwamba"** ambao kanisa linajengwa juu yake ***"wala milango ya kuzimu haitalishinda"*** **18).**

Mitume na Manabii wanajulisha siri ya Kristo.

Kisha maandiko yanasema ya kwamba kanisa, nyumba ya Mungu imejengwa kwenye msingi wa mitume na manabii (**Waefeso 2:20). Waefeso 3:5** inasema ya kwamba ufahamu wa maarifa ya Kristo ***"hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine; kama walivyo funuliwa mitume wake watakatifu na manabii".*** Mitume na manabii wanatakiwa kujulisha ufunuo wa siri kwa kanisa **Waefeso 3:3-4, 8-9).**

Ni wakati wa kuangalia tena misingi ya kanisa. Je kanisa limejengwa katika ufunuo wa Yesu Masihi? Je kanisa limepokea huduma za mitume na manabii ili kanisa liwekwe vema kwenye maarifa ya siri za Kristo? Msingi usipowekwa vyema kanisa halitaweza kushindana dhidi ya mashambulizi ya yule muovu **(Waefeso 6:11-13).**

Jiwe la pembeni

Yesu Kristo ndiye msingi wa nyumba ya Mungu, lakini Yeye pia ni jiwe kuu la pembeni. ***"naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana"*** **Waefeso 2:20b-21.** Jiwe kuu la pembeni katika jengo ndio ambayo hushikilia jengo pamoja, ikijaribiwa kwa msingi, na ni kutoka hapo ambapo jengo lote linapata sura na ***"Linaungamanishwa".*** Jambo hili la Yesu kuwa jiwe kuu la pembeni [neno hilo kihalisi 'la pembeni' kama linavyo patikana katika KJV] ni la muhimu sana.

Kumbukumbu za jiwe la pembeni katika Agano la kale zimenukuliwa katika Agano Jipya, kwa njia ya nguvu sana: **[Isaya 28:16; Zaburi 118:22; Isaya 18:14; 1 Petro 2:4-8].**

1 Petro 2:4-5 inaonyesha picha ya kanisa likijengeka. Yesu ndiye jiwe lililo hai na watu wa Mungu ni mawe yaliyo hai ***"wakijengwa kuwa nyumba ya Roho".*** Tunajengwa ndani ya Kristo Yesu, aliye jiwe kuu la pembeni; tunajengwa juu ya jiwe la msingi wa Yesu Kristo, na tunajengwa ndani ya kichwa aliye Kristo Yesu (**Wakolosai 1:18; Waefeso 4:15).**

Huduma ya uinjilisti

Mara tu mitume na manabii wameweka msingi, wakijulisha siri ya Yesu Kristo, kisha huduma ya mwinjilisti anaweza kufanya kazi vema, kuhubiri injili ya ufalme wa Mungu na kuona watu wakizaliwa mara ya pili kwa maana wamesikia mahubiri ya kuwa Kristo ni nani. Mwinjilisti anaondoka kwenda ulimwenguni kuhubiri injili **(Mariko 16:15).** Wale wanaoamini na kubatizwa **(Mariko 16:16)** wanafanyika viungo katika mwili wa Kristo **(1Wakorintho 12:13 na 18).**

Huduma ya Mchungaji

Mwinjilisti analeta waumini wapya kwa mchungaji ambaye anawaangalia, akiwalisha na maziwa ya neno la Mungu ili wapate kukua **(1Petro 2:2).** Mchungaji anawaimarisha waumini wapya katika neno la Mungu na haswa kuwafundisha kanuni za msingi ya elimu ya Kristo zilizotajwa katika **Waebrania 6:1-2.** Kama waumini wapya hawajabatizwa, basi mchungaji atashughulikia hilo pia. Pia, mchungaji atahakikisha kwamba Roho Mtakatifu ameachiliwa kwa waumini wapya [ona mfano wa Paulo katika **Mdo 19:1-6,** na yalioandikwa katika **[Mdo 8:5-17].** 'Mawe yaliyo hai' sasa yanajengwa kwenye lile jiwe la Pembeni.

Huduma ya Mwalimu

Huduma ya mwalimu ina wajibu spesheli katika kufundisha neno la Mungu, akifanya wanafunzi kutoka kwa waumini wote **(Mathayo 28:19-20).** Mchungaji anatakiwa kuwa ameanza kazi hii, lakini kimsingi hili ni jukumu la mwalimu kuwafanya wanafunzi. Waalimu, wachungaji, na wainjilisti wote wanakiwa kuandaliwa na kuwa na uelewa wa fundisho la mitume.

Paulo alikuwa akifanya mazoezi ya huduma ya mwalimu katika kanisa la Antiokia (**Mdo 11:25-26)** kabla hajaitwa na kutumwa na Roho Mtakatifu kama mtume (**Mdo 13:1-4).**

Huduma ya mitume na manabii

Tayari tumetazama wajibu muhihu wa huduma ya mitume na manabii katika kujenga kanisa katika ufunuo wa Yesu Kristo. Mara tu kanisa limewekwa kwenye msingi vyema na kuanza kufanya kazi ya uwanafunzi katika kila kanisa la mahali pamoja, basi mitume na manabii wanahitaji kuhusishwa kikamilifu katika kuleta ufunuo wa utume na unabii na kufundisha ili kanisa lote liweze kuufikia ukamilifu. Hili ndilo kusudi ambalo Yesu alitupa huduma tano zilizotajwa katika **Waefeso 4:11**

Utandaji kazi wa huduma zote ni kufanya kazi fulani ya huduma, kuwaandaa [kukamilisha] kuliweka kanisa katika mpangilio ili lipate kutenda kazi, na kulijenga [kulikuza] kanisa ***"hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"*** **(Waefeso 4:12-13).** Kanisa linatakiwa ***"kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa - Kristo"*** **(Waefeso 4:15b).** Hii haiwezi kutendeka bila mitume na manabii kufanya kazi ya huduma yao.

[Tazama Kiambatisho namba mbili]

KANISA HILI LINAKAMILISHA AJE VYOTE KATIKA VYOTE?

Ufalme wa Mungu unastahili kuja duniani

Mafundisho ya Agano Jipya iko wazi: ufalme wa Mungu unastahili uje duniani [ona ombi la Bwana **Mathayo 6:10];** Yesu ndiye Masihi, Mfalme aliyetiwa mafuta. Amekuja na Ameyapokea mataifa kama urithi wake **(Zaburi 2:7-8).** Kutokana na mamlaka yake, yaliyokamilika mbinguni na duniani **(Mathayo 28:18),** Yesu ameliamrisha kanisa Lake ***"Enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi"*** **(Mathayo 28:19)**. Tukiyatii maagizo ya Yesu kuwafanya wanafunzi, ***"tukiwafundisha kuyashika yote"*** yale Yesu aliamuru, kisha kila muumini anafanyika mwanafunzi na anafundishwa vema katika neno la Mungu, wakiwa wana uweza wa ***"Kuwafundisha wengine"*** **(2Timotheo 2:2).**

Tatizo ni kwamba kama wahuduma na waumini hawajafundishwa katika neno, wanakuja na njia ng'eni za kufanya vita vya Kiroho, pasipo kushukuru kwamba ushindi umepatikana, na kwamba kuhubiri kwa injili ya Yesu mfalme aliyepakwa [Kristo/Masihi] na ufalme wa Mungu, ni njia ambayo Mungu amepatiana ya kuona ufalme wa Mungu umeimarishwa na unafanya kazi duniani

Mungu ana mpango

Falme na mamlaka ambazo hukaa mbingu ya pili zinakuja aje katika utii wa injili hii tukufu? Falme na mamlaka zinashindwa aje? Paulo anatangaza katika **Waefeso 3:10** ya kuwa ni kupitia kanisa ambapo ***"hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho".*** Hii ni ***"Kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu"*** **(aya 11).**

Mungu ana mpango na mpango Wake tayari umewekwa vema katika Kristo Yesu. Mpango wake ni kusudi la milele: ni kwa nini Mungu aliumba? Ilikuwa ya mhimu kwa njia ipi Yesu Mwana wa Mungu kuja duniani? Ushindi wa Mfalme Aliyepakwa (Kristo) utadhihilishwa aje duniani? Maandiko inaiweka wazi: Mungu analiinua kanisa lake kuwa chombo chake ambacho kupitia kwake ufalme wake uhubiriwe na ambaye kwake ushindi utadhihilishwa. Ni kupitia kanisa lililokomaa! Ni kanisa ambalo tumeeleza kwa kifupi katika fundisho hili.

Ni kupitia kanisa

Ni kanisa linalokomaa:

- Huduma tano zinafanya kazi kikamilifu
- Kanisa lote linakua mpaka utimilifu katika Kristo,
- Ambalo limejengwa juu ya msingi wa Kristo,
- Likiungamanishwa katika Jiwe kuu la pembeni, ambalo ni Kristo,
- Na likikua katika mambo yote katika Kichwa, aliye Kristo,

Hili ndilo kanisa linalokamilika kwa vyote katika vyote!

Nguvu katika mbingu haziwezi kushindana na kanisa kama hilo

Kanisa linapokua hata ukamilifu, kwa sababu kazi ya huduma inatendeka, hizo vyombo ambazo ziko katika mbingu ya pili [ambazo ziko kati ya kanisa lililo duniani na Yesu akiwa kwenye enzi ya Mungu mbinguni], zitakuja kujua ***"kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi"*** **(Wafeso 3:10)** na falme na utawala zitaletwa katika utiifu wa neno la Mungu. Nuru ya injili inapenya giza ya himaya hiyo, na matokeo jiji, mikoa na mataifa zinaachiliwa kupokea neno la injili.

Kuna kushindana

Kuna kushindana wakati haya yanatendeka **(Waefeso 6:12),** lakini falme na nguvu haziwezi kushinda kanisa ambalo linatangaza injili na kudhihirisha tabia za wana wa ufalme. Mamlaka ya Yesu itajulikana kwa njia ya kanisa. Hii ni picha ya jinsi kanisa ambalo ni mwili wa Masihi, "***anayekamilika kwa vyote katika vyote"*** **(Waefeso 1:23)**

Tamati

Jawabu nyepesi kwa jambo ambalo ni tata na la ndani – jambo la vita vya kiroho – ni kujua na kufahamu kuwa ni mapenzi ya Mungu kwa kanisa lake lipate kuinuliwa duniani kujaza bingu ya mapepo ambayo inazunguka dunia kwa maarifa yake ya hekima ya namna nyingi.

Mpaka wakati huu, sehemu kubwa ya vita vya kiroho ambayo inafanywa na kanisa imekuwa na msingi wa ubunifu ya mwanadamu [hata maono na ndoto] na imekuwa ikifanya kazi katika nyumba ya majani. Ni wakati wa kurudi kwa neno na kuona muundo wa jengo la kanisa, nyumba ya Mungu (**1Timotheo 3:15),** imeonyeshwa vema katika maandiko.

Kusudi la Mungu hakika litakuja kutimia!

Sura ya Nne

NGAZI YA TATU YA VITA ZA KIROHO

Kanisa linaongozwa na mitume

Hii ni ngazi ya vita za kimataifa ulimwenguni kote. Hili ni kanisa ambalo linaongozwa na kuelekezwa na mitume wakisaidiwa na manabii. Kanisa la pale pale (kanisa la kijiji) ambayo tulitaza katika ngazi ya pili linaongozwa na wazee waliochaguliwa na mitume. Lakini **kanisa la kimataifa linaongozwa na mitume ambao wanabeba mamlaka ya kiserekali ya Kristo** na upako ambao unapeanwa katika kipawa cha mtume ni 'upako wa kifalme' wa Kristo mwenyewe. Kwa hivyo ni wakati mitume wako katika pahali pao pafaapo katika kanisa la Yesu Kristo ambapo kanisa lina mamlaka juu ya mamlaka na nguvu kupinga na kusimama mashambulizi ya shetani hata kupitia nguvu za kishetani kama ilivyo wakirishwa na njoka, mnyama na nabii wa uongo.

Kukabiliana na mamlaka na nguvu

Katika ngazi ya pili ya vita tulishiriki kuwa kanisa la pale pale likisimama katika mamlaka ya kiutume linaweza kujithibiti mashambulizi ya shetani kwa kutumia silaha za vita katika **Waefeso 6**. Hata hivyo, kuna mambo mengine ya ziada ya kuthibiti mashambulizi ya mamlaka na guvu na ambayo inayasababisha kukosa nguvu na kuona ya kuwa zote zimehamishwa katika upeo wa kiroho na kanisa lililo komaa la Yesu aliye Masihi.

Kitambu cha **Waefeso** kinatuambia ***"Kanisa ni mwili wake, ukamilifu wake anaye kamilika kwa vyote katika vyote"* 1:24**. Kanisa ni ukamilifu wake Kristo na kanisa litavijaza vyote katika vyote, hivyo ni, ulimwengu na haswa ikilenga upeo wa Kiroho ambao kwa wakati huu umekaliwa na mamlaka na nguvu.

Ufunuo wa siri

Katika **Waefeso 3:1-13,** Paulo anaongea juu ya kufunuliwa kwa siri, akipatiana mambo ya dani katika asili ya kweli ya kanisa linalokomaa. Kanisa lililokomaa ni kanisa ambalo limepokea ufunuo wa siri ambazo Paulo anasema zinajulikana na wale ambao wamekomaa. (**1 kor 2:6-7)** Huu ufahamu wa siri unapatianwa/unajulishwa watakatifu; ***"Ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika mataifa, nani Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu"* Wakolosai 1:27.** Paulo anatuambia ya kuwa kazi yote ya huduma ni kuwaleta watakatifu wote katika ufahamu huo, katika ufunuo huu, katika hekima kwa kuhubiri na kufundisha na kuonya kila mtu ***"tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo Yesu"* (aya 28).**

Twahitaji mitume na manabii

Paulo kwanza anatuambia ufunuo huu wa siri ulijulishwa kwake kwanza (**Waefeso 3:3),** yakuwa yalikuwa ni majira spesheli ya kipidi cha neema ambayo ilimuwezesha kuelewa na kuihubiri siri hii (**aya 2),** na siri hii ***"Wamefunuliwa mitume na manabii" (aya 5).*** Ndiposa ni ya muhimu mitume na manabii kurejeshwa na wawe huduma ya uongozi wakilileta kanisa lote katika ukomavu. Ukomavu hupatikana tu kwa kanisa kama ufahamu wa siri umefunuliwa na kujulikana.

Kuna mwili mmoja wa Kristo

Sehemu ya muhimu ya siri ni ***"Yakwamba mataifa ni waridhi pamoja nasi, wa urithi mmoja, na mwili mmoja, na washiriki pamoja nasi wa ahadi yake, iliyo katika Kristo Yesu kwa njia ya injiri"*** **Waefeso 3:6.** Mojayapo ya anguko la kihistoria ya kanisa na hiyo basi ushindi kwa shetani imekuwa ni ile nia ya 'kuwachukia wayahudi' ambayo imetafuta mizizi na kuwa katika ukristo ambapo mataifa ya kikristo na vikundi za wakristo walianza kuwa wangumu na kuhusika katika kuwatenga wengine kinyume cha mateso kinyume cha Wayahudi. Hii ni kwa sababu shetani amejua, lakini kanisa lililoko katika mwili hawayajui haya, yakuwa mwili wa Kristo utakaoinuka katika utukufu na umoja na utimilifu katika ulimwengu umejegwa na Wayahudi na watu wa Mataifa: ***"ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake"*** **Waefeso 2:15b.** Hii ni mojawapo ya matunda ya Yesu kufa msarabani na tunapo rejea ukristo wa kiutume sehemu hii ya muhimu ya siri itakuwa ya kimsingi katika kukomaa kwa kanisa: Wayahudi na watu wa Mataifa pamoja katika imani ndani ya Masihi Yesu na kuridhi pamoja baraka ambazo zimeahidiwa Abrahamu (**Mwanzo 13:26-29).**

Utajiri wa Masihi

Kisha Paulo analeta ufunuo mwingine mkuu yakuwa kupitia kuhubiri ***"utajiri wa Kristo usio pimika"*** **(Waefeso 3:8)** wote watakuja kujua ***"habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilistirika katika Mungu aliye viumba vyote"*** **(aya 9)**. Ni kwanini kuhubiriwa kwa utajiri wa Kristo ni kwa watu wa Mataifa tu? Kwa sababu Wayahudi kwa uridhi na kwa mafundisho na kwa milki yao kama watu wa Mungu, walikuwa na ufahamu wa ndani matarajio ya Masihi [Kristo] kuja na mara tu Muyahudi wa kweli amegeuka/kuokolewa kumjua Yesu aliye Masihi, hapo wanajiletea utajiri wa agano la kale neno na mafundisho ya Musa na manabii na wanaelewa kiundani kupitia Roho kutimizwa ndani ya Kristo juu ya yote waliopewa kwa njia ya kivuli na mafumbo.

Kuhamisha mamlaka na nguvu

Matokeo ya mwisho ya kanisa kujua siri ni kwamba siri inafunuliwa katika watakatifu katika undani wa ushirika ambao ni uhakika wa uwana ambapo ***"dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa BWANA, kama maji yaifunikavyo bahari"*** **Habakuki 2:14.** Maarifa haya yanapo hubiriwa na kujulikana na watakatifu, makusudi ya Mungu ni kuwa ***"Kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho, kwa kadiri ya kusudi la milele alilokusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu"*** **Waefeso 3:10-11.**

Inakuwa wazi kupitia mafundisho haya yaliyo wazi ya ajabu ya **Efe 3** yakuwa kanisa linapokuja kuijua siri kwa njia iliyokomaa na kupokea hali ya kufanyika wana - ***"Roho wa mwana wake"*** Ndani ya mioyo yetu (**Wagalatia 4:6)** – **Kuwa mamlaka na nguvu** '**zinapoteza nguvu na mamlaka.**' Zinahamishwa kutoka pahali pao katika ulimwengu wa rohoni. Hayatakuwa na mamlaka ya kuyatawala mataifa, maeneo, mji, na vijiji lakini kanisa ikileta Maarifa ya Masihi - utajiri wa utukufu - utajaa dunia na maarifa ya Masihi, YAHWEH.

ULIMWENGU WA NGUVU ZA SHETANI

Kuna ulimwengu tatu za nguvu na zimetajwa katika kitabu cha **Ufunuo 16:13-14** **"*Nikaona roho tatu za uchafu zilizo fanana na vyura, zikitoka katika kinywa cha yule joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uongo. Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu y a Mungu mwenyezi"*** Yule joka, yule mnyama na nabii wa uongo pamoja wanaunda kikundi cha nguvu tatu za uovu ulimwenguni.

Joka

"*Na yule joka akampa nguvu zake, na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi"* Ufunuo 13:2. Watu ***"wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa huyu mnyama uwezo wake"* aya 4.** Yule mnyama ni yule yule aliyefukuzwa kutoka mbinguni, ***"Nyoka wa zanani aitwaye ibilisi na shetani, aundanganyaye ulimwengu wote"* Ufu 12:9**

Yule joka amejipatiana kwa kifo na uharibifu. Kujidhihirisha kwa kimataifa kwa ugaidi katika miaka ya hivi punde kote kote ulimwenguni na kujidhihirisha kwa joka akileta kifo na uangamivu kupitia matendo ya kupendelea ya hofu. Mauaji ya haraiki ya Rwanda ya 1994 na mauaji ya kinyama ya kijamii, kabla na baada ya uharibifu, katika vita katika maeneo mbali mbali pia inaeleza wazi lengo la shetani ya kifo na uhalifu. Kalne ya ishirini na vita mbili kuu za ulimwengu ilikuwa kudhihirishwa kwa chuki ya joka kwa mwana damu. Shetani alimtumia joka, haswa Hltler katika vita za pili za dunia kuachilia kifo na uharibifu katika kiwango cha juu.

Mnyama

Ufunuo 13:1 yaongea juu ya ***"mnyama akitoka katika bahari, mwenye pembe kumi, na vichwa saba, na juu ya pembe zake ana vilemba kumi na juu ya vichwa majina ya makufuru"*** Mnyama huyu aliabudiwa (**aya 4)** alipewa mamlaka kwa muda mfupi (**aya 5).** Alinena makufuru "**atukane Mungu, na kulitukana jina lake, na maskani yake, nao wakaao mbinguni" (aya 6). "*Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda"* (aya7).** Alipewa mamlaka juu ya kila mtu na aliabudiwa na wote ila tu wale ***"majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima"* (aya 7-8).**

Mnyama anapewa mamlaka kufanya vita dhidi ya watakatifu na ana mamlaka kwa muda kuwashinda watakatifu. Mnyama amedhihirishwa kupitia serekali za wanadamu na wakati wote inatafuta kuimarisha serekali ya mpinga- Kristo watawala na miundo, hivyo ikileta mateso kanisani.

Mfano wa mnyama huyu kazini inaonekana kwa sheria zilizo pitishwa India ikipinga kubadirika kwa ukristo. Kama matokeo wachungaji wengi wamewekwa ngerezani. Kujithihilisha kwigine kwa mnyama kazini ni katika Shalia Law kwa waisiramu wenye msingi wanapopata kutawala maeneo au nchi.

Katika karne ya ishirini tulishuhudia kuinuka kwa serekali zenye nguvu za mpinga Kristo katika Jeremani na urusi. Wakati wa utawala mfupi wa Hitler Reich wa tatu, mamilioni yasiohesabika walipoteza maisha yao na uongozi wa Nazi, popote ulipohusishwa, walipinga wazi wazi kila kitu kweli na haki.

Katika Urusi vyama vya kisiasa zilizoamini juu ya mwongozo wa kiuchumi (communism) chini ya Stalin ulidumu muda mrefu kuliko Unazi na ikaadhiri mataifa mengi ya Magharibi ya Urupa na kupitia kati ya Kasikazini ya Asia, ikiwawekea miundo ya kuwafinya isio ya uungu na ikatafuta kuwaangamiza wakristo wote na misingi ya utamaduni wa mji.

Nabii wa uongo

"Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka nchi naye alikuwa na pembe mbili mfano wa mwana – kodoo, akanena kama Joka" **Ufu 13:11.** Mnyama huyu alitambulika kama **mabii wa uongo** **(Rev.16:13,19:20).** Nabii wa uongo ***"aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamshujudie mnyama wa kwanza,*** **(aya12**); ***Naye afanya ishara kubwa.*** **(Aya 13)**; ***Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi*** **(aya 14)**; ***Naye awafanya wote watiwe chapa."*** (**Aya 16**)**.**

Nabii wa uongo (mnyama wa pili) anajidhirisha katika madhehebu yote ya dunia. Huyu mnyama wa pili pia anajidhihirisha kwa aina nyingi kwa madhehebu ambayo yanaunganisha watu wengi, ambao wanajiita wakristo, katika tamaduni na mafundisho ya kanisa na imani ya kugawanyisha ambayo inanyima kanisa nguvu. Nguvu ya Jezebeli ni thihilisho ya mnyama wa pili **(Ufu 13:11)** katika mashambulizi yasio koma kwa kanisa, kwa kuingilia ngazi za kanisa.

Madhehebu yote makuu ya dunia yamedhihirisha msisimuko wa kisiasa na mafundisho ya kidini na kueneza zaidi hivi karibuni. Kumekuwa na kuinuka na kuongezeka kwa ndini za uongo.

NGUVU HIZI NI ZA KIMATAIFA SIO ZA KIMAENEO

Hizi ni nguvu za kimataifa za kishetani. Nguvu hizi hazijazuiliwa kwa maeneo au sehemu au taifa. Haziwezi kufungwa au kuharibiwa na mtu binafsi au na kanisa la pale pale. Twajua kwamba mnyama na nabii wa uongo ***"Hao wawili wakatupwa wangali hai katika lile ziwa la moto liwakalo kwa kiberiti"*** **(Ufu 19:20)** na shetani [joka] atafungwa kwa nyororo kubwa na ***"Kutupwa mpaka kuzimu, na akamfunga miaka elfu moja"*** **(Rev 20:1-3).** Hata hivyo kwa muda kanisa nilazima liandaliwe kusimama na kujidhibiti mashambulizi na kugandamizwa, mateso na adha ambazo zimeletwa na ulimwengu wa nguvu za muovu na kuonyesha na kudhihirisha ushindi wa Masihi duniani.

Maana sharti atawale

Ni wakati tu tutakapokuja katika ukomavu wa kufahamu siri ya kanisa:

- Kanisa ni nini?
- Limeketishwa wapi?
- Huo ni mwili wa Masihi ambaye tayari atamiliki kama Mfalme. ***"Maana sharti atawale yeye, hata aweke maadui wake wote chini ya miguu yake"*** **1 Wakorintho 15:25,** yakuwa maadui wa Masihi watashindwa na kanisa.

Kristo anangojea katika enzi yake mpaka hayo yatakapo tendeka. Hapo ndipo atakapo achiliwa kutoka mbinuguni **(Mdo 3:21)** na adhihirishwe katika kuja kwake [kurudi]

Mbingu zilizofunguka

Kutoka wakati wa ubatizo wa Yesu, na isipokuwa tu siku tatu kutoka kufa kwake na kufufuka, **Mbingu zilifunguka na haziwezi kufungwa.** Kihistoria ni dhambi zilimtoa mtu kutoka kwa Mungu na hivyo ikamruhusu adui kutawala na kumiliki hapa ulimweguni kwa nguvu zake iwe ni katika vijiji, mikoa, taifa au mataifa.

Kwakuwa Yesu alikuwa ni mwana wa Mungu asiye na dhambi mbingu zilimfungukia katika ubatizo wake (**Mt 3:16-17, Lk 3:21-22)** na akapokea utimilifu wa Roho wa Mungu. Pia wazi wazi alitambuliwa kama mwana wa Baba. Natangia msalaba na ufufuo, damu ya Yesu imekuwa juu ya kiti cha enzi mbinguni **(Ebr 9:11-14, 24, 10:19-22).** Mbingu zimefunguliwa daima na haziwezi kufungwa tena kwa sababu ya damu ya Kristo iliyo juu ya kiti cha rehema.

Kumfikia bila kizuizi

Hata hivyo katikati ya mbingu za Mungu, Mbingu ya tatu (**2 Kor 12:12),** Kuna mbingu ya pili ambapo nguvu na mamlaka **(Kol 1:16)** na shetani, "***Ikiwa ni viti vya enzi, au ushulutani, au enzi au mamlaka"*** zinadumu na zinatawala juu ya wana wakutotii **(Efe2:2)** Sisi kama wana wa ufalme tunaishi ulimwenguni katika mbingu maridadi mbingu ya kwanza [Jua, mwezi,na nyota] lakini tunamfikia Mungu bila vikwazo kupitia damu na Roho. (**Efe 2:13, 18).**

Kwa kuwa tumeketishwa katika mbingu za tatu katika Kristo, Shetani na nguvu zake hawawezi kutuondoa kutoka kwa Mungu kama ilivyo wezekana katika agano la kale – kumbuka ilibidi Danieli kumngonjea malaika Gablieli siku ishirini na moja kumletea jawabu kutoka kwa Mungu (**Dan 10:13). Huu ni mpango ulio na umuhimu mkubwa sana.** Kama hatusadiki hayo, tunakoseshwa kupigana na kujaribu kufunga nguvu katika ulimwengu wa pili. Pia tunawalaumu kwa yale yote yanatendeka wakati kanisa haifanyishi mamlaka kazi na utawala kama vile Kristo ametutuma.

Ni wakati wa kupokea Roho wa kufanyika wana

Niya muhimu kufahamu yakuwa haikuwa mpaka Yesu alipofika katika utimilifu katika maisha yake hapa ulimwenguni ambapo aliweza kupokea Roho wa kufanyika Mwana katika utimilifu na kutembea katika mbingu zilizo funguka, akiongozwa na Roho kikamilifu, akijua kikamilifu juu ya mapenzi ya Baba yake.

Kwa hivyo ni wakati tu kanisa litakapofika katika ukomavu lote mwisho wa nyakati ambapo tutaweza kuridhi utimilifu wa Roho ya kufanyika mwana na kutembea chini ya mbingu zilizo funguka kikamilifu na kuongozwa na Roho na kuyatambua mapenzi yake.

Kanisa limetumwa kuyafikia mataifa

Niwakati tu mitume na manabii wanaongoza makanisa ya taifa na mataifa, yaliyowekwa kwa mpangilio sawa, ndio kanisa litainuka tena kuwa nguvu za kimataifa na nguvu za Kiungu ambazo zitabadilisha mataifa, mji, na vikundi vya watu kwa Bwana Yesu Kristo. Hata hivyo, maandiko yanatuambia mnyama atakuwa na mamlaka kushinda watakatifu kwa muda na kuwaua baadhi yao. Hii imetabiliwa katika **Danieli 7:21, na Ufu 13:7.** NIkatika kipindi hiki cha nguvu za mnyama ***"Subira na imani ya watakatifu"*** **(Ufu 13:10)** zitadhihirishwa na ushindi wa watakatifu utakuwa mkuu hata kupitia kufia dini. Watakatifu wataridhi ufalme **(Lk 12:32)** na falme zota za dunia hii zitakuwa za Bwana na za Masihi wake **(Ufu 11:15).**

KIKUNDI CHA KIUTUME

Katika nyakati za urejesho ambao tuna fulsa ya kuishi, Mungu ameweka wakfu kuudwa kwa vikundi vya kiutume duniani kote. Kikudi cha utume ni:

- Mwili wa watakatifu ambao wameitwa pamoja katika kujitoa.
- Kuona ufalme wa Mungu umedhibitishwa hapa duniani miongoni mwa mataifa.
- Watakatifu hawa wameitwa kutoka kwa idara na miungano katika kutembea katika utiifu sawa wa Kristo na neno la Mungu.
- Katika vikundi hizi huduma zote na vipawa ambazo Mungu amepeana katika agano jipya zapata nafasi yake na kujieleza kamili.
- Vikundi hizi zinatanda katika mataifa; zinaongozwa na mtume ama mitume.
- Zikiwa na tabia sawa kwa kila mshiriki akiwa na ufahamu mzuri wa mwito wa Mungu na ufunuo wa nguvu za uwana.

Kundi la kwanza la kiutume

Mfano wa kwanza wa kundi la kiutume ni waamini mia moja na ishirini katika chumba cha juu katika **Mdo 1**. Kikundi hiki kilikuwa kikundi **kilicho chaguliwa cha wanafunzi wakiwa na nia moja, wakiendelea na maombi na sala;** ni kwa kikundi hiki Mungu alituma Roho Mtakatifu.

Mitume ambao Yesu aliwafunza walikuwa **tayari na kujiandaa kupokea kwa kikamilifu Roho wa uwana** na walikuwa na uwezo wakuhudumu katika kiwango sawa na Yesu. Ujuzi wa **Mdo 2** kwa kundi la kiutume katika chumba cha juu ulikuwa tofauti sana na ujuzi wa waamini wapya (3000) ambao walibatizwa siku hiyo na kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Ujuzi wa wale 120 ulikuwa tofauti sana na kujazwa na Roho Mtakatifu ambao mataifa walipokea katika nyumba ya Kornelio (**Mdo 10)** ama kujazwa kwingine (mabatizo) ya Roho Mtakatifu katika kitabu cha matendo ya mitume.

Ufufuo wa kipentekote ambao ulianza mapema karne ya ishirini na umeendelea toka urejesho wa kujazwa ama kubatizwa na Roho mtakatifu. Haukuwa urejesho wa utimilifu wa roho wa uwana. Roho wa uwana unarejeshwa siku hizi!

Ni wakati wa ukomavu, sio wakati wa pentekote. Mwisho pentekote ni moja ya misingi lakini uwana ni njia ambayo kanisa lililokomaa linafikia hatima yake, **ambayo ni utukufu wa Kristo ukidhihirishwa kwa watakatifu wake katika dunia.**

Mungu anainua makundi ya kiutume

Vikundi vya kiutume ndio viongozi ambao Mungu anainua katika siku hizi kuonyesha kwa watu wake ushindi ambao ametupea juu ya pepo na shetani. Vikundi vya kiutume vinapoanza kufanya kazi katika ukamilifu wa mamlaka ya Masihi hapa duniani hivyo makundi ya waamini watafulika kukumbatia utume na kanisa hatimaye litakuja katika hatima yake: Kutawala na kutamalaki pamoja na Yesu aliye Masihi Katika Sayuni.

Kikundi cha kiutume ni muundo kwa kanisa

Katikati ya mwaka wa 2001 Bwana ulituagiza kuunda kikundi cha kiutume na kwa miaka ametuangazia kwa ufahamu na utendaji wa kikundi cha kiutume. Kikundi cha kiutume kinainuliwa na Bwana watu walio ***mfano/kielelezo.***

Paulo anatazama haya katika **Wafilipi 3:15-17** ambapo anaongea kwa wale ***"wakamilifu"*** tuwaze hayo, na kuenenda katika ***"lilo hilo".*** Mapema katika **2 Kor2: 6-16**, Paulo anataja ***"hekima ya Mungu katika siri "***ambayo ni ya wale waliokomaa kupokea na hekima hii ***"Mungu aliiazimu tangu milele kwa utukufu wetu".***

Mungu amekusudia kanisa kufikia ukomafu na niya muhimu kanisa kufikia ukomavu ili kuweza kupokea ufunuo wa siri na lianze kuhisi na kutembea katika utukufu wa Bwana.

Katika siku hizi za mwisho mtazamo wa **'kanisa'** umekuwa wa kuchanganyisha sana wengi wakitaja jengo, au dhehebu au idara kama Kanisa. Kwa hivyo Mungu anainua haswa vikundi vya kiutume kuwa mfano wa kanisa la Agano jipya.

Tabua kwamba Paulo asema ***"sisi tunayo nia ya kristo"*** **(1 Wakorintho 2:16)!** Ni uhakika kwa wingi! Hakuna mshiriki mmoja wa mwili atakuwa na "**nia ya Kristo"** wakiwa peke yao lakini ni uhakika wa wote.

Nitukiwa kikundi (Mwili yote) ambapo kanisa litamshinda shetani.

SILAHA TATU ZA MUHIMU - Ufu.12:11

Shetani na mapepo wake walifukuzwa

Maandiko yanatuambia ya kuwa shetani alishindwa na mikaeli na malaika wake na ***"akatupwa hata nchi, na malaika wake wakatupwa pamoja naye"*** **(Ufu. 12:7-9)**

Ufalme wa Mungu na nguvu za Masihi wake zimekuja.

Kisha maandiko yasema sauti kubwa ikasikika ikisema "***sasa kumekuwa wokovu, na nguvu na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mstaki wa ndugu zetu, yeye awastakiye mbele za Mungu mchana na usiku"*** **aya 10**

Swali: kulingana na andiko hili shetani **alitupwa chini lini?**

Jawabu: Alitupwa chini wakati ambapo **ufalme wa Mungu** uliimarishwa pamoja na nguvu za Masihi wake?

Swali: Haya yalitendeka lini?

Jawabu: Wakati kristo alifufuka toka kwa wafu.

Kristo alifufuliwa na ***"na ubora wa ukuu wa uweza wake"*** wakati alipo "***Mfufua katika wafu, akamuweka mkono wake wa kuume katika ulimwegu wa roho"*** **Efe 1:19-20.** Nikupitia msalaba ambapo Yesu ***"akiisha kuzivua enzi na mamlaka"*** **Wakolosai 2:15.** Shetani alishindwa na akapoteza msimamo wote katika ulimwengu wa rohoni msalabani.

Kupitia kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo, kanisa limeinuliwa na ***"kuketishwa pamoja naye katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu (kwa neema tumeokolewa)"*** **Efe 2:5-6.** Kama matokeo kanisa, likiwa hapa ulimwenguni lakini limeketishwa katika ulimengu wa rohoni, lina uwezo kumshinda mstaki wa wandugu ambaye sasa yuko katika upeo wa ulimwengu akitustaki.

Silaha tatu

Zipo silaha tatu au njia tatu ambazo kanisa linaweza kushinda shetani na hizo njia zote ziko katika mazingira ya mwili wote. ***"Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa"*** **Ufu 12:11.**

Kwa damu ya Mwana-kondoo

Katika somo kutoka **Ufunuo. 12:11**, imekuwa dhahili kuwa, ushindi juu ya shetani, mstaki wa wandugu, unawezekana tukiwa kanisa mwili wote wa waumini, ukishikamanishwa vyema, utamshinda. Maandiko yasema ***'walimshinda'.*** Niwakati tu watakatifu wameshikamanishwa katika kikundi cha kiutume – watu ambao ni kielelezo ambao wamejipatiana kutembea katika ukomavu – ambapo ***"damu ya Mwana –kondoo"*** inafanya kazi kuwapatia watakatifu huo ushindi

Damu ya Mwana kondoo inafanyaje kazi?

1 Yohana 1:7 Inatuambia, ***"Tukieneda nuruni, kama vile yeye alivyo katika nuru' twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote"*** Ndugu zangu, niya muhimu sana kutembea pamoja katika nuru ya Yesu kristo, tukiongozwa na Roho wake Mtakatifu katika nuru ya neno, tukiwa wazi, tukiheshimiana na upendo wakushirikiana na kunyenyekeana mmoja kwa mwimgine katika kumcha Kristo.

Kulingana na **Efe 5:18-21** maisha yaliyo ya kunyenyekea kwa ndugu katika kumcha Mungu, ni ishara ya maisha yaliyojaa Roho. Kwa hivyo wakati wowote ambapo mangumu,

kutokubaliana, kutokupatana au shida ingine kati ya wandugu, lazima hesabu iwe fupi sana na tupatane kwa haraka mmoja na mwingine katika kumcha Kristo.

Hivi ndivyo **"damu ya Kristo Yesu"** inafanya kazi katika mwili: Wakati wowote shida [dhabi] inainuka inatakikana ishugulikiwe mara moja kwa toba na kukiri, tukiruhusu damu ya Kristo itakase. Kwa hivyo uhusiano katika mwili unarejeshwa kwa muda mfupi, tukiruhusu ushirika wa kweli na kuwawezesha watakatifu kutembea kaitka nuru pamoja.

Ijapokuwa ni uhimu kwa kila mtakatifu kutembea katika nuru ya Yesu kristo, ni lile jambo la pamoja na kudhihirika ambalo Mungu anatazamia- kwa kanisa kutembea katika ukomavu- na nikujieleza kwa pamoja ambako kutamshinda mstaki wa wandugu, Kukipatiana kwa washiriki wote katika ushirika kutembea katika ushindi.

Kwa neno la ushuhuda wao

Pili walimshinda mstaki wa wandugu ***"Kwaneno la ushuhuda wao".*** Tazama tena ni kukili kwa pamoja, ***'ushuhuda wao'.*** Hii inatupeleka tena katika **Wafilipi 3:15-17** ambayo inadhihirisha asili ya umoja kwa kanisa lililokomaa: ***"Basi sisi tulio wakamilifu natuwaze hayo, na hata mkiwaza mengine katika jambo lote … mnifuate mimi, mkawatazame wao waendao kwa kuufuata mfano tuliowapa ninyi"*** hebu natuwe ***mfano!*** Mungu anainua mwili wote- kikundi cha kiutume:

- Ambao watakuwa ni watu kielelezo
- Ambao watakuwa wa ***"moyo mmoja na roho moja"***
- Ambao watashika ***"Mambo yote kwa pamoja"***
- Ambao watapatiana ***"Ushuhuda wa kufufuka kwa Bwana Yesu kwa nguvu."***
- ***"Na neema kubwa itakuwa juu yao wote"*** **(Mdo 4:32:33)**

Watu kama hao wana ushuhuda wa pamoja!

Kukiri

Katika Spirit filled Bible the Kingdom Dynamics chini **Warumi 10:9** inagusia neno ***'Kukiri',*** ambalo limetoka kwa neno la kiyunani '*homologeo'* Ina picha ya *kujenga matangazo ya hadhara ambapo uhusiano uliokubaliwa inaimarishwa kwa makubaliano',* Neno hili linamaanisha '*kunena neno moja'*. **Ebr 3:1** Inahimiza umuhimu wa kuwa tumemkiri Yesu mtume wetu [huku kumkiri Yesu kumekosekana kanisani kwa miaka1800]

Neno la ushuhuda wao

Huku ndiko kukiri kwa mitume:

- ***"Imani wali*yokabidhiwa watakatifu mara moja tu" Yuda 3**
- **Ni ushuhuda wa ufahamu wa siri (Efe 3:2-5)**
- **Ushirika wa siri (3:8-11)**
- **Uhakika wa kufanywa wana (Efe 1:5)**

Ni kwa kikundi, kanisa kwa jumla, ambapo Mungu anatupa "***nia ya Kristo"* (1 Kor 2:16).**

Kwa hivyo neno la ushuhuda wetu ni ufahamu wetu na kukili kwetu ya kuwa sisi ni wakina nani:

- **Mwili wa kristo**
- **Wateule wa Mungu**

- **Watakatifu walioitwa kwa wito mkuu (Wakifikia kufufuliwa kwa wafu Wafilip 3:11) Na kusudi la Mungu ambalo** amekamilisha ndani ya Kristo Yesu **(Efe3:11)** Nainakuja kutimia katika kanisa la siku za mwisho.

Ushuhuda huu ni ***"Hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi"*** ambayo "**itajulikana na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho" (Efe 3:10).** Waweza sasa kuona vile mwili wote unatembea katika ushindi, ukimshida mstaki wa wandugu? Ni kanisa ambalo limefikia ukomavu, likisha pokea hekima ya ndani ya neno la Mungu

Hawakupenda maisha yao hata kufa

Tatu walimshinda kwa ***"kutoyapenda maisha yao hata kufa".*** Huu ndio utendaji wa **1 Yohana 3:16 "*Katika hili tumelifahamu pemdo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajiri ya hao ndugu."*** Kutoyapenda maisha yetu hata kifo inaongea kuhusu kujitoa kwetu katika ushirika, kwa kundi la kiutume na kufurahia mahali petu katika mwili wa Kristo, ***"tulinunuliwa kwa dhamana".*** Gharama ya mwisho ni kufia dini, na kufia dini sio tu' kufa kwa imani' lakini ni kuyatoa maisha yetu kwa marafiki zetu.

Siku za hivi punde Bwana ameweka wazi kwetu yakwamba anataka sisi ***'Kuitoa mioyo yetu kwake na kwa mmoja na mwingine'.*** Hii ndio asili ya kikundi cha kiutume. Nimeutoa moyo wangu kwa ndugu zangu. Wandugu wameitoa mioyo yao. Kama uhakika wa ***"Kutoyapenda maisha yao hata kufa"*** unajulikana kwetu, uhusiano wa kijitoa kwetu ambao tunafurahia unakuwa kizuizi chenye nguvu ambacho kinatukinga kutokana na mashambulizi ya yule muovu, ambayo mara nyingi yanakuja kama mastaka.

Usindi kamili unapatikana kwa kanisa laYesu Kristo sasa. Kupitia kifo chake na kufufuka, Yesu ametimiza mapenzi yaliyopangiwa ya Mungu na sasa kanisa "***ambalo ni mwili wake",*** sasa limeketishwa ***"Pamoja naye katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu,"*** ili ***"katika zamani zinazokuja audhihirishe wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo"*** **Efe 2:6-7.**

ONYO LA MUHIMU

Onyo la muhimu na maelezo yakuleta kwa kanisa wakati huu ni kama yafuatayo: **hakuna maelekezo katika Agano jipya au mamlaka kwa kanisa ama kwa mtu binafsi au vikundi yakitafuta 'kufunga' na 'kuangusha'** mamlaka **na nguvu katika ulimwengu wa roho juu ya mji, maeneo, au mataifa.**

Mafundisho mengi ambayo yanajulikana katika vitabu na kwa njia zingine za kuelekeza kanisa 'kupigana vita' na lamani za maeneo ya kiroho **Sio mafundisho ya Biblia** hata kidogo. Hakuna uhakika kwa injiri au kwa nyaraka ambapo Yesu ama mitume wanatufundisha au kutuonyesha matendo kama hayo na vita za kiroho za aina hiyo. Watu wamekuwa na mawazo ya aina yote na kupigana vita za aina nyingi za kiroho ambazo zinaonekana kuwa nzuri kwa wakati na kuonekana kama zimedhibitishwa katika Roho lakini hazijadhibitishwa katika neno la Mungu. Niwakati wa kanisa kurudi kikamilifu kwa mafundisho ya kiutume, kwa ushuhuda wazi wa maandiko.

Kama matokeo ya mafundisho mabaya **Wengi wamekiuka katika maeneo ya vita za kiroho.** Kumekuwa na jaribio nyingi za kufunga mamlaka na nguvu. Muda na nguvu zimetolewa kutafuta ufahamu wa ngome za kishetani na mizizi ya uovu uliyofichwa na mengineyo katika maisha ya watu binafsi, katika historia ya mji, maeneo na mataifa. Makanisa mengi na watu binafsi wameenda hasara na shida zingine kama magonjwa, pamoja na kopooza, katika kuwa

wazimu na pia vifo zizizo za wakati. Makanisa mengine na wachungaji wengine wameangamizwa kwa sababu wametoka katika mapenzi ya Mungu na kukeuka kwa mipaka ya adui.

Tumekuwa hatuja komaa, bila kutumia hakili zetu za kiroho ***"kupabanua mema na mabaya"*** **(Ebr 5:14).** Twahitaji kufunzwa tena elimu ya msingi ya Kristo (**Ebr 5:12-6:3).**

Tumepuuza siri na ufunuo wa ajabu ya kwamba ni kupitia ***"kuhubiri utajiri wake Kristo usio pimika; na kuwaangazia watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilistirika katika Mungu aliye viumba vitu vyote, ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho; kwa kadiri ya kusudi la milele alilo likusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu"*** **(Efe 8:3-11)**

TAMATI

Kitabu hiki ni utangulizi na tamati ya fundisho ya vita za kiroho na mamlaka ambayo Kristo amewapa waamini kama washiriki wa mwili wake kanisa.

Tumeonyesha kwa kifupi maeneo ya mamlaka ya kibinafsi, kanisa la pale pale (lililo wekwa kwa mpangilio wa kiutume) maeneo ya mamlaka, na upeo wa kimataifa, ambapo tu ni kanisa ambalo linatembea katika ufunuo wa siri na mamlaka ya uwana, likiongozwa na mitume na manabii wanaofanya kazi vyema, wanaweza kusimama na kupinga mashambulizi ya shetani. Tukikiuka nje ya maeneo ya upeo wa mamlaka yetu tunaweza kuteseka kwa mashambulizi isiyofaa na kupata uhalibifu katika maisha yetu, katika kanisa letu, au pia katika ngazi za kitaifa na kimataifa.

Kwa njia ingine, tunapokuja kujua kwa ufunuo na kumtii Mungu:

- Ukuu wa mamlaka na nguvu zake na
- Kupitia Kristo- Masihi anayetawala – amepatiana hayo mamlaka na nguvu kwa kanisa, tutahisi ushindi mkubwa na tuanze kutembea katika upeo wa "***Kufunuliwa kwa wana wa Mungu" Warumi 8:19.***

Tutatembea katika ufunuo wa siri ya Kristo na kanisa lake na tutajua ufunuo wa kanisa lililo ketishwa pamoja na yeye katika ulimwengu wa roho.
Tutakuja kuelewa mamlaka tuliopewa kupitia utume ambayo kwa hakika ni jia ya Agano jipya kutimiza mamlaka ya kwanza ya uumbaji katika **Mwanzo 1:28.**

"Mungu akawabariki, Mungu akawaambia zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi".

USHINDI WA MWISHO NI MWILI WOTE KUSHINDA NA KURIDHI VITU VYOTE KAMA WANA WA MUNGU.

SURA YA TANO

KUTEMBEA KATIKA USHINDI

Wengi wetu ambao wemeokoka, ambao wanajua kwamba tumezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, tunajipata **hatuishi katika ushindi**. Hii ni changa moto ya kudumu kwa waumini. Neno la Mungu lasema tuna ushindi kupitia Yesu na ya kwamba tunaweza kuishi na kutembea katika ushindi huo. Ni naandika haya kuleta himizo kwetu, ili tuimarike zaidi vyema katika neno la Mungu, tukitaka ***"Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni, huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu"*** **Wakolosai 3:16.**

YESU AMEMHARIBU SHATANI

Neno la Mungu linasema ***"Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa"*** **Waebrania 2:14-15**

Yule ambaye ndiye chanzo cha shida zetu ameshughulikiwa. Ibilisi ameshindwa! Ndio, yeye ***"Kama simba angurumaye, huzunguka -zunguka, akitafuta mtu ammeze"*** **(1Petro 5:8),** lakini Yesu amemharibu, hivyo ni, kumpokonya mamlaka yake – Yesu alisema, ***"Ninazo funguo za mauti, na za kuzimu"*** **(Ufunuo 1:18).**

Kwa sababu Yesu amemshida shetani, tunaweza kumpinga shetani kwa kuwa watiifu kwa Mungu ***"naye atawatoroka"*** **(Yakobo 4:7).** Kwa sababu Yesu ameharibu ***"kazi za ibilisi"*** **(1Yohana 3:8b),** tunaweza ***"kumpinga, huyo, tukiwa dhabiti katika imani"*** **(1Petro 5:9).**

Ushindi ni kwa imani

"*Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu – mwenye kuushinda ulimwengu ni nani, Isipokuwa ni yeye aaminiye ya kwamba Yesu ni mwana wa Mungu?"* **1Yohana 5:4-5**

Lakini si vyepesi hivyo? Ama ni vyepesi! Shinda ambayo tumekuwa nayo, ni kwamba tumekuwa hatuamini ni vyepesi! Biblia inasema ushindi ni kwa imani. Ni vyepesi kama kumuamini Yesu, kuwa yeye ni Mwana wa Mungu. Kwamba yeye ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili na kwamba kupitia kifo chake na kufufuka Kwake Amemshinda shetani na kumharibu yeye aliyekuwa chanzo cha shinda zetu.

Wanafunzi ambao Yesu alituma katika **Luka 10** walikuja wakifurahia, wakisema ***"Bwana, hata pepo wametutii kwa jina lako"*** **aya 17.** Wanafunzi hao walipata uzoefu wa mamlaka ya jina la Yesu.

Hakuna mkristo ambaye anatakiwa kusumbuliwa na mapepo. Kama Yakobo asemavyo ***"Basi mtiini Mungu, mpingeni shetani, naye atawakimbia"*** **(Yakobo 4:7).**

Tatizo ni kutotii

Ni kwa nini wakristo hawatembei katika ushindi? Ni kwa sababu hatulitii neno la Mungu kama lilivyoandikwa. Hakika hatuliamini neno la Mungu.

Maandiko yanasema ***"ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uweza wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi"*** **Waefeso 2:2**

Hii ilielekeza katika kundanganywa kwetu na kujiendesha kwetu ***"katika tamaa za miili yetu, tulipotimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu, watoto wa hasira kama na hao wengine"*** **(Waefeso 2:3).** Wengi wetu wanapitia shinda na **tamaa za mawazo-** tunapatwa na mawazo yasio ya haki na tunafungwa katika fikira zetu.

Maandiko yanasema ***"Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi; kila atendaye dhambi hakumwona yeye, wala hakumtambua, watoto wadodo, mtu na asiwandanganye; atendaye haki yuna haki, kama yeye aliye na haki"*** **1Yohana 3:6-7.** Kumbuka ya kuwa haki ni kwa imani na imani huja kwa kusikia na kusikia neno la Mungu **(Warumi 10:17)**

Ushindi dhidi ya mamlaka na nguvu

Katika miongo ya hivi punde katika ukristo, kumekuwa na himizo ya vita za kiroho na wengine wameshauri vibaya na wakatoka kwenda kwa vita na mamlaka na nguvu.

Habari njema ni kwamba hata mamlaka na nguvu zimepata kushindwa kabisa na Yesu. Maandiko yanasema, "***akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akazishangilia katika msalaba huo"*** **Wakolosai 2:15.** J.P Green anatafsiri aya hii kama *'akiisha kuvua wazi enzi na mamlaka, akajionyesha (Kwa hayo) kwa hadhara akishangilia (juu yake). '**Yake'** ni **msalaba.***

Kama vile kwa hakika shatani ni adui aliyeshindwa ambaye tunao ushindi kamilifu, hivyo navyo pia enzi na mamlaka, ule utawala wa giza na majeshi ya waasi katika maeneo ya mbinguni **(Waefeso 6:12)** wameshindwa na Yesu juu ya msalaba. Imekuwa ni ushindi wa hadhara. Lakini zitajaribu kushawishi yeyote atakaye amini, kwamba hazijashindwa na zinashikilia enzi na mamlaka na nguvu juu ya mataifa, na jiji na miji.

Waumini ambao wanaamini kulingana na neno la Mungu kama lilivyo andikwa, hawadanganyiki kamwe na ibilisi; hawako chini ya nguvu na mamlaka ambayo ameweka.

Yesu ameketishwa juu

Wakati nguvu kuu za Mungu ***"Aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho,"*** Yesu alipaa mahali pa mamlaka yote. Aliketi "***juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na ushultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katike ule ujao pia"*** **Waefeso 1:20-21.**

- Mungu "***Amevitia vitu vyote chini ya miguu yake"***
- Mungu ***"Amemweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa"***
- **Kanisa, [ambayo ni sisi] "*ndio mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote"* aya 22-23**

Mungu alizisamehe dhambi zetu na akatufanya kuwa hai katika Kristo kupitia kuzaliwa upya. Hii ilikuwa kwa sababu ya upendo wake mkuu "***kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda"*** **(Waefeso 2:1-4).**

Ulijua ni kwa sababu ya upendo wa Mungu mkuu kwako alikuokoa. Anasema "***Naam, nilikupenda kwa upendo wa milele, ndio maana nimekuvuta kwa fadhili zangu"*** **Yeremia 31:3.**

Alituokoa kwa neema yake na "***akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa rohoni katika Kristo Yesu"*** **(Waefeso 2:5-6).**

Hebu ukweli huu mwepesi wa maandiko ya Agano Jpya iwe 'mkate na siagi' ya imani yako na acha imani ya neno la Mungu liwe ndilo la kuendelesha maisha yako.

Usimtazamie shetani

Wakati mwingine watu wakiwa na tatizo, wanataka kumulaumu shetani na wanataka kutafuta ‘ni roho ipi inawagandamiza? Ama ni nguvu gani ninapigana nayo? Maswala yote mawili si sawa! Tunatakiwa kumpinga shetani, lakini kwanza tumtii mungu.

Yesu alituambia tumwombe Baba, tukimuuliza ***“lakini tuokoe na yule muovu”*** **(Luka 11:4).** Tuna uweza wa ***“nanyi mpingeni huyo, mkiwa dhabiti katika imani”*** **(1 Petro 5:9).**

- Usitiwe hofu na shatani;
- Lakini wacha Bwana Yesu awe wa kuogopwa na wa kuhofia!
- Usiisikize njama za nadharia!
- Lakini acha neno la Mungu liwe timanzi ya maamuzi yako.

Neno la ushuhuda

“*Msiseme, Ni fitina, katika habari za mambo yote ambayo watu hawa watasema, Ni fitina; msihofu kwa hofu yao, wala msiogope. BWANA wa majeshi ndiye mtakayemtakasa; na awe yeye hofu yenu, na awe yeye utisho wenu. Naye atakuwa ni mahali patakatifu; bali ni jiwe la kujikwaza na mwamba wa kujikwaa kwa nyumba za Israeli zote mbili”* {Kwa njia nyingine, kwa wale wanaamini katika njama; wale ambao wameweka imani yao kwa roho na nguvu watajikwaa; na kuwa na ungumu kumpata Mungu!}

Kwa maana watu wanaamini katika njama, “***wengi watajikwaa juu yake, na kuanguka na kuvunjika, na kunaswa na kukamatwa.***

Uufunge huo ushuhuda, ukatie muhuri sheria kati ya wanafunzi wangu. Nami nitamtazamia”. Ushuhuda na sheria zote zikizungumzia neno la Mungu: twatakiwa kuwa na ushuhuda! Na tunatakiwa kujua neno lafundisha nini!

“Nami nitamngojea BWANA, awafichaye uso wake nyumba ya Yakobo; na nitamtazamia. Angalieni, mimi na watoto hawa niliopewa! **{**Tazama nukuu katika **Waebrania 2:13}.**

Sisi tu ishara na ajabu katika Israeli, zitokazo kwa BWANA wa majeshi, yeye akaaye katika mlima Sayuni” **Isaya 8:12-18**

Watu ambao wanamcha Mungu, hivyo ni, wanaoamini neno lake,

watakuwa kama ishara katika Israeli.

Watu kama hao watasimama hata miongoni mwa watu wa Mungu.

Watakuwa watu ambao watatembea katika ushindi. Wapendwa kuna ushindi!

Ni kwa njia ya imani na tunaweza kutembea kwa imani katika Ushindi.

Sura ya sita

SHUHUDA ZA VITA ZA KIROHO KATIKA NGAZI ZOTE TATU

Kwa miaka mingi kama mhuduma wa Yesu Kristo nimekuja kujua binafsi kwa ujuzi uhakika wa vita za kiroho katika ngazi zote tatu ambazo nimekuwa nikifunza katika nakala hii. Nimejifunza yakuwa kunazo hatari katika kila ngazi ambazo twatakiwa kuwa makini juu yake ili tuwe na hekima na kubabanua na kuto kudhuriwa.

UJUZI KATIKA NGAZI YA KWANZA KATIKA VITA ZA KIROHO

Kama muhuduma mchanga mapema miaka ya 1980, dada alikuja kwangu akaniambia Bwana amemuonyesha ya kwamba kuna pepo katika maisha yake na akaniuliza kuitoa. Nilikuwa na uhakika wa mamlaka yangu ndani ya Kristo kutenda hayo na kwa **kuitikia ombi lake na kwa kujitakia kwake kukili nakuwa huru, kwa wepesi nikaamrisha pepo amtoke**. Kulikuwa na kujidhihirisha kidogo pepo alipotoka na dada akahisi kufunguliwa papo hapo, akijua ya kuwa pepo ametoka.

Yesu alisema "***Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajiria" Mathayo 12:28.*** Kila mara ninapo kemea pepo binafsi kutoka kwa mtu kumekuwa na ujuzi wa upako wa Roho Mtakaifu na mamlaka ya ufalme wa Mungu unadhihirika.

Ujuzi huu wa mapema miaka 1980, ulikuwa wa nguvu sana na nikaondoka nikifurahia. Nilipokuwa nikiendesha gari nikielekea nyumbani kutoka kwa jengo la kanisa jioni hiyo mara tu baada ya ukombozi, jambo ng'eni na lakusubua likatandeka barabarani: Bila onyo dereva aliyekua akija kutoka upande mwingine aligeuka mbele yangu na kuzuia kugongana kichwa kwa kichwa ilibidi nisimamishe gari kwa nguvu. Ilikuwa tu ni kwa sababu nilikuwa mashambani na nikiendesha kwa mwendo wa pole ambapo hatukugongana. Kilicho subua kilikuwa kwamba dereva huyu mwingine alikuwa chini ya utawala wa pepo na ilikuwa ni jaribio la kuniharibu kwa sababu ya ushindi wa ukombozi jioni hiyo. Mwanzo nilitishwa sana na nikawa katika hali ya mshangao na nikajua kuwa hayo yalikuwa ni majibizano kutoka kwa pepo. Kisha nikatubu kuwa sikuwa na ***"kiasi na kukesha"*** baada ya ushidi wa ukombozi **(1 Petro 5:8).**

Uwe makini kuwa kila **mara tunapo pokea ushindi dhidi ya shetani atajaribu kuleta majibizano kinyume chetu.** Atajaribu kutudhuru na tunapo endelea kujifunza njia ya vita za kiroho kuna mazoea ya kupuuza nguvu za mapepo. Yesu alisema, alipowapa wanafunzi mamlaka yote dhidi ya adui, yakuwa "***hakuna kitu kitakacho wadhuru" (LK 10:19).*** Hata hivyo hakusema shetani hatajaribu.

Kwa hivyo ujilinde, haswa baada ya tukio la vita za kiroho ambapo umefanya madhara katika ufalme wa giza.

Kumuweka huru mwanamke kule Pakstani

Katika mwaka wa 2005 nilikuwa na kikundi Pakstani, na jioni moja, nilikuwa mnenaji katika mkutano wa nje wa injiri katika hema kubwa ambayo iliwekwa kwa sababu ya mikutano. Mamia ya watu walihudhuria mukutano wa usiku, na mara tu tulipo kuja kwa jukwaa,

tulimtambua mwanamke aliyekuwa na pepo, akivutia hisia za watu katika mkutano. Kikundi changu kikaona hayo na wakaanza kuomba na kufanya maombezi na tabia za pepo zikakoma nikaweza kuhudumu. Mwishoni mwa mkutano palikuwa na mwaliko wa uponyanji wa wagonjwa na watendakazi wakaanza kumbeba yule mwanamke na kumleta mbele. Katika mkutano, Mungu aliweka uhakika ndani ya moyo wangu yakuwa huyu mwanamke atasetwa huru. Hata hivyo niliwaagiza watendakazi kumchukua mwanamke nyuma ya kongamano kwa kuwa pepo ulimsubua tena pepo alipojaribu kuvutia hisia za watu tena na kutatiza uponyaji wa wengine.

Tulipotoka kwa mkutano, nilimwendea yule mwanamke mwenye pepo na akafunguliwa kwa haraka kwa kumfunga pepo aliyekuwa ndani yake, kwa jina la Yesu, na kumfanya mwanamke akubaliane nami, nikinena jina la Yesu na kuiamrisha itoke. Pepo alitoka; tulimsimamisha yule mama kwa miguu yake na tukamwombea kujazwa na Roho Mtakatifu na akaongea lugha ya mbinguni. Mwanake huyu alikuwa na pepo tangu akiwa mtoto. Watu haswa wachungaji wa kijiji waliokuwa nasi walishangaa. Wachungaji walisema ‘hatujaona jambo kama hili! Huu ndio muujiza mkuu ambao tumeona!’

UJUZI WA NGAZI YA PILI YA VITA ZA KIROHO

Katika mwaka 1989 nilikuwa mchungaji wa kanisa ndogo katika kijiji chetu, ambalo nilikuwa nimepanda awali. Nilikuwa nimepokea mafundisho yenye msingi katika **Isaya 43:5-7** juu ya kuwaita waridhi wa wokovu’ kutoka kasikazini, kusini, mashariki na magharibi. Katika kifungo hiki cha maandiko, neno la Mungu linanenea kasikazini likisema “***Nitaambia kaskazini toa, nayo kusi, usizuie; waleteni wana wangu kutoka mbali, na binti zangu kutoka mbali”*** **aya 6.** Mafundisho niliyoyapokea, yalionyesha yakuwa yule pepo ‘mtu mwenye nguvu’, nguvu za pepo katika mbingu katika kila upande, zilikuwa na nguvu juu ya watu walioishi kutoka upande huo na kupitia vita za maombi ya kiunabii, sisi kanisa tunaweza kuamuru hizo nguvu ‘kutoa’ watu wa Mungu waje kanisani.

Bwana aliniita katika kipindi cha maombi ya kufunga na kuomba mwezi wa nane na tisa mwaka wa 1989 na nilikuwa naendelea kunenea nguvu za kasikazini katika mji wetu kulingana na mafundisho haya katika kitabu cha **Isaiya**. (Kanisa letu lilikuwa kasikazini mwa mji). Siku moja nikiwa nimezama katika maombi ghafla ni kagundua **nilikuwa nikiona katika ulimwengu waroho nikaona enzi kuu ya shetani ikiwa na mtawala aliyeketi juu yake.** Nilishangaa nani kashtuka, kutoka kilindi cha moyo wangu na sikujua nifanye nini. Hapakuwa maneno yaliyonenwa nanikarudi mara kutoka kwa maeneo hayo.

Baadaye siku hiyo hiyo nikaendesha gari langu na nikahusika katika ajali mbaya mno. Ajali hiyo haikutarajiwa: Gari likatokea upande wangu wa kuria nalikaniingilia. Sikuumia; gari halikuharibika vibaya lakini Roho Mtakatifu alinijuza kwamba **Ilikuwa ni roho wapepo aliyejaribu maisha yangu.**

Kutoka siku hiyo mambo yasio ya kawaida yakaanza kutendeka kwa ushirika wa kanisa. Wandugu wapendwa waliokuwa wakitembea nasi na kufanya huduma nasi wakaja kwangu wakasema ‘tutaondoka kwa kanisa’ hawakuwa na sababu kamili au machungu; hawakukusudia kwenda katika ushirika mwingine. Kisha baada ya majuma machache familia zingine zikaondoka na tukaanza kung’ang’ana. Pesa zikapunguka na ilinibidi kwenda kazi ili nipate kuongezea mapato yangu. Tulifahamu hiyo ilikuwa kazi ya nguvu za mapepo lakini hatukujua tusimame namna gani. Hii ilikuwa sababu hatukuwa katika mpangilio wa kiutume. Nilikuwa sehemu ya dini ya kipentekote lakini **hapakuwa na kivuli cha kweli cha kiroho.**

Tangia wakati huo huduma yangu na ushirika wa kanisa hilo ukaanza kudidimia na mwezi wa kumi 1990, nilifunga ushirika huo na nikajiuzulu kutoka kwa huduma nikashindwa; nikajihisi nilikuwa nimeshindwa! Lakini Mungu hakuniona kama nimeshindwa na baada ya miaka mitatu Mungu akanirejesha kwa huduma kunitayarisha kwa huduma kuu ya kiutume ambayo alikuwa amenipangia tangia mwanzo.

Nilikuwa nimekiuka upeo wa vita za kiroho?

Nimejiuliza swali hili mara nyingi. Hata hivyo sijawahi shawishika kwamba nilikiuka bali ninaamini kuwa nilikuwa nilianzisha; yakuwa Mungu alikuwa akinipa ujuzi wa kwanza ili niwafundishe na kuwaongoza wengine. Sikuwa nimewekwa katika mpangilio wa kiutume kwa maana nilikuwa sina ufahamu wa huduma ya utume wakati huo.

Baada ya miaka kumi na miwili mwaka wa 2001 nilikuwa nikifanya kazi katika huduma ya kiutume na tulikuwa tumepokea mtume mwingine kule SHILOH. Alipotutembelea mara ya kwanza aliongozwa na Bwana kuniwekea mikono mbele ya umati na kutangaza mbele ya nguvu na mamlaka yakuwa mimi nilikuwa mtume wa Yesu Kristo. Hili lilikuwa nitangazo la nguvu nami, na mashahidi waliokuweko, wakahisi nguvu na mamlaka zilizo dhibitishwa na kuwachiliwa kwangu kama mtume. Hapo awali Bwana alikuwa amenionyesha kwamba **huduma ya kiutume inabeba 'upako wa kiufalme' wa Kristo** na mitume wanapo rejeshwa kanisani kanisa litakuwa na mamlaka juu ya nguvu na mautawala.

Muda mfupi baada ya mtume kutembea, sisi katika SHILOH tuliongozwa kufunga siku tatu kumtafuta Bwana kwa kutuelekeza kama huduma. Alituonyesha kuwa tutaenda katika mlima uliokuwa katika kaskazini mwa mji wetu na tukabiliane na hiyo enzi na mtawala wake wakipepo ambayo ilinipinga na kuniletea uharibifu na ushirika wa kanisa miaka 12 hapo awali. Watu kumi miongoni mwetu tulikutana kwa mlima asubuhi na mapema na nikafanya matangazo ya nguvu na tukapuliza barangumu (talumbeta ya pembe ya kondoo) na kisha tukasherehekea meza ya Bwana. Palikuwa na muamini mpya pamoja nasi na kwa wakati huo akapokea maono. Maono aliyoyaona ni yale yale niliyoyaona miaka kumi na mbili hapo awali. Akasema kama nilivyo litangaza neno la Mungu na ukuu wa Kristo, mtawala katika ile enzi aliyeyuka kama mushumaa na akashuka chini kutoka kwa enzi. Kisha enzi ikaripuka kwa vipande nyingi na pia akaona mguu mkubwa, ukiwa na kiatu, ukishuka kutoka Mbinguni na ukasaga vile vipande zikawa mavumbi. Halleujah!

Bwana alikuwa akituonyesha kuwa kanisa likimpokea mtume na liwekwe katika mpangilio wa kiutume, basi kanisa liko na mamlaka sio tu ya kupinga nguvu na tawala lakini kuona wakiwa wametapanywa na pia wakiwa wameharibiwa.

Toka tukio hilo la ujuzi wa mwaka wa 2001 mwezi wa kumi, Nimetembea miji mingi ya Austaralia na baadhi ya mataifa ya ng'ambo, kwa ujasiri nikitangaza kuwa mimi ni mtume wa Yesu Kristo na **nimejua yakuwa mamlaka na nguvu zinanitii katika Jina la Yesu.**

UJUZI KATIKA NGAZI YA TATU YA VITA ZA KIROHO.

Katika mwaka wa 2002 nikuwa nikisafiri Kenya na mashariki ya Uganda na kuhubiri katika miji tofauti. Tulikuwa tumepitia Mauritius tukielekea Kenya na Mauritius nilikasirishwa na tabia za hadhra za baadhi ya Waislamu. Kumuona mwanamme Mwislamu akitembea mitaani hatua mbili au tatu mbele ya mke wake, kichwa cha mke wake kikiwa kimefunikwa ila hali ameinama, kwangu ilionekana kuwa tabia ambayo haina maana na haikubariki, na pia sio tangazo nzuri la dini.

Pia miji ya Afrika ya Mashariki, kulikuwa na misikiti na mapema asubuhi tungeamshwa na maombi ya juu. Haya yalitendeka katika mji ambayo asli mia tisini ni wakristo. Ijumaa kulikuwa na mahubiri siku nzima, kutoka kwa mskiti na vyombo vya kupasa sauti, wakiwashambulia wakristo na injiri. Zaidi nikakasirishwa na kujionyesha huku kwa hadhara kwa dini ya mtu mwingine hata katika mji uliojaa wakristo.

Nilianza kuhubiri kwa wakristo waamini Mungu kuwa na mji ambao hauna msikiti au waislamu wawaheshimu wakristo na waishi kwa amani na wakristo walio wengi, sio kila mara kujaribu kuwaletea ndini yao ya Uislamu. Sikufikiria kuwa nimeenda zaidi. Haswa kama mgeni na muhuduma wa injiri, ilionekana haipo katika mpangilio **na hari iliyopita mipaka ambapo walio wachache waliinua sauti zao wakieneza maombi na mafundisho yao kwa watu ambao hawakuichagua dini yao.**

Sikutambua kikamilifu kuwa nilikuwa nikipingana na nguvu za shetani za ulimwengu wote. Hata hivyo katika safari nikawa mgwonjwa sana malaria na nikalazwa hospitalini Dar-es-salaam. Daktari aliyenipokea aliniambia kuwa nimeambukizwa kwa hali ya juu sana. Niliwekwa maji na kwa siku mbili nilikuwa mgonjwa sana.

Katikati hali hiyo ya kusumbuka mawazo kwa nguvu nilipo kuwa mgonjwa, **mjumbe wa shetani kwa mfano wamalaika aliyeanguka (mfano wa mtu) akanitokea na akaninenea.** Akasema kitu kama ‘watakiwa kuondoka nje ya Afrika; rudi Australia. Lazima uachane na waislamu na ujari mambo yako.’ Maneno haya yalinenwa kwa mamlaka lakini sikuhisi uoga na wakati nilipona kutokana na malaria na nikakutana na kikundi, kwa haraka tulijipanga na kwa neema ya Mungu tukajipatiana tena kwa kazi ambayo Mungu alikuwa ametuitia katika Afrika ya mashariki.

Kwa hakika imekuwa tangia wakati huo yakwamba kazi ya kiutume ilifunguka na ikakua na nguvu sana Kenya na tangia wakati huo imepata mizizi Uganda, Rwanda, Burudi, Kongo ya kati na Tanzania.

Ilikuwa baabaye mwaka wa 2003, ambapo Mungu alinipa ufahamu kwamba bila kukusudia, **Nilishambulia na nikashambuliwa na nguvu za shetani za dunia yote.** Nilikuwa nimekeuka? Pengine kwa kiwango yakuwa niliongea kinyume cha uwepo wa misikiti na vyombo vyao vya kuhubiri, nilikuwa sina hekima na heshima. Ilikaribia kuchukua uhai wangu lakini Mungu alinikomboa kabisa. Hata wakati wa mashambulizi, wandugu walionipokea kule Afrika ya mashariki waliamini ilikuwa ni shambulizi na jambo la kuhuzunisha yakuwa ugonjwa wangu, kikundi changu kilitambua kuwa ni mashambulizi ya kiroho. Ninaamini kwamba Mungu aliiruhusu, tena, kwa ujuzi wangu. Nikiisha kuponea mashambulizi hayo sasa nimehekimika na ninababanua zaidi katika upeo huu wa vita za kiroho na ninaweza kupatiana uongozi wakiutume kwa kanisa.

Wakati huo mmoja wa wana wangu wa kiutume aliye katika mashariki ya Kenya kwa wakati huu anaushindi katika kuwafikia Waislamu, hata wahubiri. Kuingia kwake nikatika heshima na shukrani kwa Waislamu, kwa amani akishiriki nao na kuwafikia na ufahamu wa Koran, lakini wakati huo huo akiwauliza maswali juu ya Koran na haswa Koran inasema nini juu ya Yesu.

Nguvu za shetani zilizo tafuta kuniua ni nguvu za ulimwengu wote na roho iliyo nyuma ya Islamu ni nguvu nyingi za roho ya mpinga - Kristo. Wakati sio Waislamu wote wanaofanya kazi kwa roho hii, twahitaji kutambua roho tunayopigana nayo, tunapotafuta kuwafikia Waislamu.

Watu ambao wamepitisha kiasi katika imani ya Kiislamu ambayo haivumilii dini zingine na inahimiza kuenea kwa Uislamu kwa nguvu ni mfano wazi wa nguvu tatu za shetani za ulimwengu wote zote zikifanya kazi pamoja. **Joka ndiye anayechochea uharifu** ambayo inashawishi Waislamu kuwa wauaji wa mabomu ikikusudia kuwaua watu wengi iwezakanavyo wasio na hatia.

Wakati Waislamu wanaopita kipimo wanapata nguvu za siasa katika mataifa, waingiza **Sharia law** ambayo ni njia yao ya serekali za wanadamu. Serekali za aina hii zinagandamiza kabisa na wanaamuru mabadiriko yaliyozidi ya maisha ya dini. **Hii ni kuonekana kwa mnyama katika serekali za mpinga- kristo.**

Zaidi ni kudhihirika kwa **kazi ya nabii wa uongo katika dini ya kiislamu kwamba wanaamini maandiko ya mtu mmoja na maandiko yake mengi yanapinga Mungu na Bibilia na neno lake.**

Yesu alisema wazi baada ya kufufuka kwake **"*Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani"* Mathayo 28:18.** Injiri kwanza ilihubiriwa katikati ya dini ya [Kiyahudi] ambayo ilikuwa kali na wengi waliwekwa korokoroni na wengine wakapoteza maisha yao kwa sababu ya kuhubiri na matendo yao ya imani ya Kikristo. Kisha mitume na wanafunzi walipoondoka nje ya utawala wa Rumi na hata na zaidi kwa injiri, miji yote na mataifa walipokea kwa nguvu.

Mwisho wa nyakati, Ukristo wa kiutume unainuka tena na falme zingine zote za dunia hii zitavamiwa na injiri na hatimaye injiri itapata ushindi ufalme wa Mungu unapoimarishwa katika kila taifa, miongoni mwa kila kabira na lugha.

Vita vya maneno

Njia ambayo shetani anashindwa ni kwa nguvu ya neno la Mungu. Wakati shetani alipomjaribu Yesu njangwani, alitumia maneno, hata maneno yaliotoka kwa Biblia. Yesu alimshinda shetani kwa kutumia maneno: ***"imeandikwa!"*** Nyuma ya matumizi ya neno kwa njia yenye nguvu ni maombi. Petero anatupatia mwelekeo mkamilifu katika **Mdo 6:4** ***"na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile neno."***

Kwa njia fulani tunaweza kusema vita vya dunia ya pili ilishindwa kwa maneno. Maneno ya Winston Churchill yalikuwa na nguvu sana kuliko maneno ya Adolf Hitler! Twafahamu yakuwa Churchill na Britain kuu waliungwa mkono na nguvu na maombezi ya kuendelea ya kikundi cha watakatifu katika Wales ambao Mungu alikusanya pamoja na Rees Howells [mpaka 100] katika Swansea. Waombezi hawa waliomba kwa masaa manane kila siku kwa miaka sita ya

vita na rekodi iliwekwa ya mizigo na kisha ushindi ambao ulikuja katika chumba cha maombi ambao pia ulifanyiwa kazi katika uwaja wa vita.

Tulipo ongozwa na Roho kukabiliana na nguvu za pepo juu ya mashariki ya nchi yetu katika mwaka wa 2001, tulitumia maneno! Mbinu sawa tuliopewa kwa neno la Mungu ni kutangaza, kuhubiri, kutabiri, na kutangaza neno lake! Neno ni kweli (**Yohana 17:17)**

Amen!